MODULI

# Njia za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili

# KIU 07322

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu
Shahada ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi – Kwa njia ya Masafa

# Hakimiliki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya kazi hii kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima isipokuwa kwa kunukuu matini fupifupi zinazoweza kutumika kwa ajili ya utafiti na mapitio ya maandiko.

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, 2022

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**Shahada ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi – Kwa njia ya Masafa**

S. L. P. 20679,
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
**Dar es Salaam**
Simu: +255 22 2150838
Baruapepe: info@iae.ac.tz
Tovuti: www. iae.ac.tz

## Shukurani

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dkt. Michael Ngumbi anapenda kutoa shukurani za dhati kwa watu mbalimbali ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine katika kukamilisha kazi hii. Wafuatao ambao ni wafanyakazi wa TEWW wanastahili kutajwa kipekee kwa kuongoza mchakato huu hadi kukamilika kwake.

| | |
|---|---|
| Julius E. Challigha: | Mkuu Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu |
| Rose E. Isaka: | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mwandishi) |
| Eric Samba: | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mhariri) |

……………………………

Dkt. Michael W. Ng'umbi

**Mkurugenzi**

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

# Yaliyomo


**Kuhusu moduli hii** 1

Muundo wa moduli hii ... 1
Marejeleo ... 1

**Maelezo ya jumla kuhusu moduli** 3

Karibu katika moduli hii ... 3
Umahiri wa Jumla ... 3
Mbinu za usomaji ... 3
Je, unahitaji msaada? ... 4
Mazoezi ... 4

**Namna ya kutumia moduli hii** 5

Ishara za pambizo ... 5

**Somo la Kwanza** 7

Kuandaa Somo la Kiswahili kwa Wanafunzi Watu Wazima ... 7
Utangulizi ... 7
Matokeo ... 7
Kuchambua Vijenzi vya Mtaala ... 7
Chimbuko la Muhtasari ... 8
Uchambuzi wa Maazimio ya Kazi ... 16
Uchambuzi wa Andalio la Somo ... 17

Sifa za mwalimu wa Kiswahili 18

Tafakuri ya Somo ... 22
Zoezi la Somo ... 22

**Somo la Pili** 23

Maandalizi ya Mwalimu ... 23
Utangulizi ... 23
Matokeo ... 23
Silabasi ... 23
Udhaifu wa Silabasi ... 25
Maazimio ya Kazi ... 25
Tafakuri ya Somo ... 49
Zoezi la Somo ... 49

**Somo la Tatu** 50

Kuchambua Mbinu Mahususi za Kujifunzia na Kuwezeshea Somo la Kiswahili kwa Darasa la Watu Wazima ... 50
Utangulizi ... 50

Matokeo ... 50
Dhana ya mbinu za kufundishia Lugha ... 50
Mbinu za Kufundishia Lugha ya Kiswahili kwa darasa la watu wazima ... 51
Mbinu nyinginezo za kufundishia na kujifunzia Lugha ... 63
Tafakuri ya Somo ... 68
Zoezi la Somo ... 68

**Somo la Nne** 69

Kutumia Mbinu Mahususi Katika Kuwezeshea Stadi za Somo la Kiswahili kwa Darasa La Watu Wazima ... 69
Utangulizi ... 69
Matokeo ... 69
Kufafanua na Kuwezesha Somo la Ufahamu ... 69
Kufafanua na Kuwezesha Somo la Utungaji ... 74
Kufafanua na Kuwezesha Somo Ufahamu wa Kusoma ... 78
Kufafanua na Kuwezesha Stadi za Kusikiliza ... 81
4.5 Kuwezesha Stadi za Kuzungumza ... 83
Tafakuri ya Somo ... 85
Zoezi la Somo ... 85

**Somo la Tano** 86

Kuandaa Zana za Kuwezeshea Somo la Kswahili kwa Darasa la Watu Wazima ... 86
Utangulizi ... 86
Matokeo ... 86
Dhana ya Zana za Kuwezeshea ... 86
Aina mbalimbali za Zana za Kujifunzia ... 87
Makundi ya Zana za Kuwezesha ... 88
Sifa za Zana za Kuwezeshea ... 88
Faida ya Zana za Kuwezeshea ... 89
5.6 Umuhimu au Manufaa ya zana za Kufundishia na Kuwezeshea ... 89
Tafakuri ya Somo ... 90
Zoezi la Somo ... 90

**Somo la Sita** 91

Kupima Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili ... 91
Utangulizi ... 91
Matokeo ... 91
Maana ya Upimaji/Tathmini ... 91
Aina za Upimaji way Somo la Kiswahili ... 92
Mbinu na Zana za upimaji (Vifaa vya Upimaji) ... 93

Tafakuri ya Somo ........ 94
Zoezi la Somo ........ 94

**Maswali ya Marudio na Majadiliano** 95

**Marejeleo** 97

# Kuhusu moduli hii

Moduli hii ya kutumia Stadi za Uandishi katika Maisha imetayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Moduli zote zilizotayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima zina muundo linganifu, kama ilivyoelezwa hapa chini.

## Muundo wa moduli hii

### Maelezo ya jumla kuhusu moduli

Maelezo ya jumla kuhusu moduli hutoa utangulizi wa jumla wa moduli. Habari zinazopatikana katika maelezo ya jumla kuhusu moduli zitakusaidia kuamua:

- Kama moduli hii inakufaa;
- Kile unachohitaji kukijua;
- Unachoweza kutarajia kutoka katika moduli; na
- Muda utakaohitaji kutumia ili kukamilisha moduli.

Maelezo haya ya jumla pia hutoa mwongozo juu ya:

- Mbinu za usomaji;
- Mahali pa kupata msaada;
- Mazoezi ya nyumbani na tathmini ; na
- Ishara za vitendo mbalimbali.
- Masomo.

Tunatilia mkazo kuwa usome maelezo ya jumla kuhusu moduli hii kwa makini kabla ya kuanza masomo yako.

### Yaliyomo kwenye moduli

Moduli hii imegawanywa katika masomo manne. Kila somo lina:

- Utangulizi wa yaliyomo kwenye moduli;
- Matokeo ya somo;
- Maudhui ya kimsingi ya somo pamoja na mazoezi mbalimbali ya kufanya;
- Muhtasari wa somo; na
- Mazoezi  na tathmini, kama inavyohitajika.

### Marejeleo

Kwa wale wanaopenda kujifunza mengi juu ya mada hii, tunawapa orodha ya marejeleo ya ziada mwishoni mwa Moduli hii. Marejeleo haya yanaweza kuwa vitabu, makala au tovuti.

## Maoni yako

Baada ya kukamilisha Moduli ya Stadi za Uandishi katika Maisha, tutashukuru ikiwa utatenga muda wako kutoa maoni yako kuhusu kipengele chochote cha moduli hii. Maoni hayo yanaweza kuhusu:

- Yaliyomo kwenye moduli na muundo wake;
- Makala za kusoma kwa moduli na marejeleo mengine;
- Mazoezi ya nyumbani ya moduli;
- Tathmini za moduli; na
- Muda wa moduli.
- Usaidizi katika moduli (wahadhiri waliosimamia moduli, usaidizi wa kiufundi, n.k.).

Ukitoa maoni mwafaka utatusaidia kuboresha moduli hii.

# Maelezo ya jumla kuhusu moduli

## Karibu katika moduli hii

Mpendwa mwanachuo, moduli hii inahusu Njia za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Imeandaliwa kama mwongozo na rejea kwa wanachuo wa Shahada kwa Njia Huria na Masafa katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Moduli imegawanyika katika masomo sita ambayo ni: kuandaa somo la Kiswahili kwa wanafunzi Watu Wazima, maandalizi ya ufundishaji, kuchambua mbinu mahususi za kujifunzia somo la Kiswahili, kutumia mbinu mahususi stadi za somo la Kiswahili kwa wanafunzi Watu Wazima, kuandaa zana za kuwezeshea somo la Kiswahili na kupima ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi watu Wazima. Kila somo lina kazi na mazoezi ya kutosha yatakayokufanya uelewe vizuri yaliyomo kwenye moduli nzima. Ni matumaini yangu utafurahia kujifunza moduli hii.

## Umahiri wa Jumla

Baada ya kumaliza kujifunza moduli hii utaweza kuchambua na kutumia njia za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi watu wazima.

## Mbinu za usomaji

Kwa kuwa wewe ni mwanafunzi wa Elimu ya Watu Wazima kwa Njia Huria na Masafa, utaratibu wako wa kusoma utakuwa tofauti na ule ulioutumia ulipokuwa ukisoma katika mfumo rasmi. Utachagua unachotaka kusoma, utakuwa na motisha ya kitaalamu na/au ya kibinafsi inayokusukuma, na bila shaka utakuwa ukiratibu shughuli zako za kiusomaji huku ukizingatia majukumu yako mengine ya kitaalamu au kijamii.

Kimsingi, utakuwa unayadhibiti mazingira yako ya masomo. Kwa hivyo, utahitajika kufikiria juu ya masuala ya utendaji yanayohusiana na udhibiti wa wakati, kuweka malengo, udhibiti wa shinikizo na kadhalika. Pengine utahitaji kujizoesha tena katika maeneo kama upangaji wa muda, namna ya kuimudu mitihani, na kutumia mtandao kama marejeleo ya ujifunzaji.

Mambo utakayozingatia sana ni *muda* na *nafasi*, yaani muda unaotenga kwa masomo yako na mazingira unamosomea.

Tunapendekeza kwamba uitumie nafasi hii – kabla ya kuanza kujisomea kibinafsi – kujifahamisha mambo haya.

## Je, unahitaji msaada?

Mpendwa mwanafunzi, katika mchakato wako wa kujifunza, unaweza kuhitaji msaada kuhusu mambo mbalimbali. Kwa mfano, mahali unapoweza kupata msaada na namna ya kupata msaada huo. Pamoja na hayo, unaweza kuhitaji ufafanuzi kuhusu moduli unazosoma. Hivyo basi, unashauriwa kuomba ufafanuzi wa yote hayo kwa mratibu wa kituo chako au mwezeshaji wako. Pia, unaweza kufungua tovuti ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima yenye anwani hii: www.iae.ac.tz au piga simu hii +255 22 2150838.

## Mazoezi

Baada ya kila somo, unahitajika kujibu maswali ya zoezi la somo. Majibu ya zoezi hili la kila somo hautayawasilisha kwa mwezeshaji wako, ni kwa ajili ya kufanya tafakuri ya ulichojifunza. Pia, utapewa majaribio na mazoezi ambayo utayafanya na kuyawasilisha kama utakavyoongozwa na mwezeshaji wako. Pamoja na hayo, utatakiwa kufanya mitihani ya majaribio kwa ajili ya upimaji wa maendeleo yako ya kitaaluma.

# Namna ya kutumia moduli hii

## Ishara za pambizo

Wakati unajifunza moduli hii utagundua kwamba kuna matumizi mengi ya ishara za pambizo. Ishara hizi zina jukumu la kuashiria aina fulani ya matini, kazi mpya au kubadilika kwa zoezi. Zimetumiwa ili kukuongoza kujua namna ya kuitumia moduli hii.

Seti nzima ya ishara imetolewa hapa chini. Tunapendekeza kuwa ujizoeze ishara hizi na maana zake kabla ya kuanza masomo yako.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Zoezi | Tathmini | Zoezi la Nyumbani | Kisa Mafunzo |
| Mjadala | Zoezi la Kikundi | Usaidizi | Kumbuka! |
| Matokeo | Kusoma | Tafakari | Mbinu za Usomaji |
| Muhtasari | Istilahi | Muda | Kidokezi |

# Somo la Kwanza

## Kuandaa Somo la Kiswahili kwa Wanafunzi Watu Wazima

### Utangulizi

Sura hii inalenga kumuelekeza mwalimu vifaa ambavo atatumia katika kumwezesha mwanafunzi mtu mzima vikiwemo, mtaala, muhtasari, azimio la somo na andalio la somo. Hivyo katika sura hii mwanafunzi anatarajiwa kuwa na uwezo wa kubainisha mabo mahimu na kuandaa somo la Kiswahili. Katika uandaaji wa somo la Kiswahili kwa watu wazima, yapo mambo, zana na vifaa mbalimbali vya kufundishia ambavyo mwalimu au mwezeshaji anapaswa kuwa navyo. Vifaa hivi humuongoza mwalimu katika kufikia malengo aliyoyakusudia ili kuleta matokeo mazuri katika tendo la ujifunzaji. Mwalimu anapaswa kuandaa mambo ambayo mwanafunzi anapaswa kujifunza, mada, vitabu pamoja na mbinu za ujifunzaji. Ili kuwezesha somo la Kiswahili, mwalimu anapaswa kuwa na mtaala, silabasi au muhtasari unaonyesha mada zitazofundishwa, azimio la kazi, andalio la somo, vifaa vya ufundishaji. Hivyo, mpendwa mwanafunzi, hebu tuone na tuchambue vitu vya msingi ambavyo mwalimu anatakiwa kuvifanya au kuwa navyo na kuviandaa kabla tendo la ufundishaji na ujifunzaji halijaanza.

### Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kuchambua mtaala wa somo la Kiswahili;
- Kuchambua muhtasari wa somo la Kiswahili;
- Kuandaa azimio la kazi; na
- Kuandaa andalio la somo.

### Kuchambua Vijenzi vya Mtaala

- Kufafanua dhana ya mtaala
- Kueleza uhusiano wa mtaala, sera na mipango mikakati ya kitaifa
- Kuchambua muhtasari wa Kiswahili kwa kuelezea ubora na udhaifu wa mihtasari ya Kiswahili

- Kuelezea maana ya azimio la kazi
- Kuanisha viambajengo vya azimio la kazi
- Kuandaa azimio la kazi
- Kuelezea faida za azimio la kazi
- Kuelezea maana ya andalio la somo
- Kubainisha vimbajengo vya andalio la somo
- Kuandaa andalio la somo
- Kuelezea faida za andalio la somo

Muhtasari wa mada zinazopaswa kufundishwa katika somo fulani kwa muda wa mwaka mmoja kwa darasa mahsusi.

## Chimbuko la Muhtasari

Silabasi hukuzwa kutoka kwenye mtaala wa masomo. Nchini Tanzania, silabasi hutayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Tanzania kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Taasisi ya Elimu Tanzania hukuza silabasi tofauti katika kila somo, huku ikiongozwa na malengo ya elimu ya taifa. Hivyo basi, somo la Kiswahili lina silabasi mbili muhimu. Muhtasari wa Kiswahili kwa shule za upili daraja la chini kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, muhatasari uliokuzwa mara ya mwisho mwaka 2005. Pia, kuna muhtasari wa Kiswahili kwa elimu ya upili daraja la juu kwa kidato cha tano hadi cha sita uliokuzwa mara ya mwisho mwaka 2009. Nchini Kenya, muhtasari wa Kiswahili ni mmoja kwa ajili ya kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule za upili. Utofauti huu unajitokeza kwa sababu ya mifumo ya elimu za nchi hizi, Tanzania ikutumia mfumo wa elimu 7:4:2:3 na Kenya mfumo wa elimu 8:4:4.

**Mambo ya kuzingatia katika ukuzaji wa silabasi ya Kiswahili**

a) Silabasi inapotayarishwa, lazima itilie maanani malengo ya elimu ya taifa. Kila mada inayopendekezwa katika silabasi ni sharti ichangie kufanikisha malengo ya taifa. Kwa mfano, ikiwa lengo la elimu ya taifa ni kujenga na kudumisha misingi ya kuthamini umoja, amani na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, wakuza silabasi wanapaswa kupendekeza kwa waalimu kufundisha vifungu fulani vy ufahamu vinavyokuza uzalendo au kupendekeza vitabu vya fasihi vinavyokuza uzalendo.

b) Mada zinazozingatiwa katika silabasi lazima zitilie maanani uelewa wa mwanafunzi wa wastani katika kila darasa. Kwa

hivyo, mada zinazopendekezwa zinapaswa kueleweka kwa mwanafunzi wa kiwango cha wastani. Hii ina maana kuwa mada husika zisiwe ngumu sana au sahili sana.

c) Mada yoyote inayopendekezwa kuzingatiwa katika silabasi, inahitaji kutilia maanani mazingira ya mwanafunzi wanaokusudiwa.

d) Uelewa awali wa wanafunzi ni muhimu katika utayarishaji wa muhtasari wa Kiswahili. Wanaotayarisha silabasi wanastahili kujiuliza, "Je, kiwango cha uelewa wa wanafunzi tunaowaandalia silabasi kikoje?" Kwa mkabala huu, mada zitakazozingatiwa katika silabasi ya kidato cha kwanza, yatazingatia mambo ambayo yalifundishwa katika darasa la saba.

e) Uundaji wa silabasi sharti uzingatie matakwa na mahitaji ya kila mwanafunzi binfasi na jamii kwa jumla. Hii ni kwa sababu silabasi haiwezi kukuzwa katika ombwe tupu.

f) Ubunaji wa silabasi lazima utilie maanani kiwango cha ukuaji wa mwanafunzi. Hii ni kwa sababu, mada zitazofundishwa katika viwango tofauti vya wanafunzio vinapaswa kuenda sambamba na ukomavu wa akili. Wanafunzi wa kidato cha kwanza watafundishwa mada sahili tofauti na wanafunzi wa kidato cha nne. Hili linatokana na ukweli kuwa akili za wale wa kidato cha pili hazijakomaa zikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha nne.

g) Silabasi inapokuzwa lazima itilie maanani muda utakaotumiwa kufundisha mada mbalimbali katika kila kiwango. Silabasi haipaswi kushirikisha mada nyingi ambazo hazitaweza kufunika kwa muda uliyotengwa. Ikiwa muda uliotengewa mada fulani kufundishwa ni mfupi, walimu watafundisha kwa haraka haraka ili waweze kuhitimisha kazi yao, lakini wanafunzi hawataelewa ipasavyo.

h) Silabasi inapoandaliwa inahitaji kuzingatyia masomo yale mengine. Hii ni kwa sababu, masomo mbalimbali hutegemeana na kyulingana. Kwa mfano, somo la Kiswahili linakopa baadhi ya mambo kutoka kwenye somo la kiingereza. Pia, fasihi ya Kiswahili ina mambo ya

kuzingatia katika fasihi ya kiingereza na masomo mengine kama Falsafa na Elimu Jamii.

## Vipengele vya silabasi ya Kiswahili

Katika sehemu hii, silabasi ambayo itarejelewa ni silabasi ya kidato cha kwanza hadi cha nne nchini Tanzania. Kabla ya mwalimu kuanza kuandaa maazimio ya kazi, anashauriwa kwanza, kutangamana na silabasi vya kutosha. Silabasi ya Kiswahili kwa kidato cha kwanza hadi cha nne hubeba vipengele vifuatavyo:

a) Malengo ya elimu nchini Tanzania.

b) Madhumuni ya elimu ya upili.

c) Ujuzi wa jumla wa somo la Kiswahili.

d) Malengo ya jumla ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili.

e) Muundo wa muhtasari. Kimsingi, muhtasari wa Kiswahili kwa kidato cha I-IV, una sehemu mbili kuu ambazo ni: utangulizi ambao unasheheni jalada, jina, hatimiliki, yaliyomo na utangulizi wa muhtasari, na sehemu ya pili inajumuisha yaliyomo au yatakayofundishwa kwa kila kidato, mbinu za kufundishia na zana zitakazotumiwa katika uwasilishaji wa somo.

f) Muda wa mafunzo,

g) Taratibu za upimaji wa somo.

h) Upambanuzi wa yatakayofundishwa katika kila kidato ujuzi utakaopatikana na wanafunzi wa kila kidato na pia, malengo ya kufundisha kiswahuili katika kila kidato.

Muhtasari wa Kiswahili kwa shule za upili kwa kidato cha kwanza hadi cha nne hauna tofauti kubwa inayojitokeza ikilinganishwa na kiwango cha tano hadi sita, isipokuwa jinsi mipangilio ya mada mbalimbali inavyojitokeza katika silabasi zote mbili. Labda, tofauti inayojidhihirisha ni kuwa muhtasari wa Kiswahili kwa shule za upili kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, haupambanui taratibu za upimaji wa somo la Kiswahili kama ilivyo katika muhtasari wa kidato cha tano hadi cha sita.

## Utoshelevu wa Silabasi ya Kiswahili

Silabasi ya Kiswahili imekuzwa kwa manufaa ya wanafunzi wa shule zote za upili nchini. Takriban mada zote ambazo

zingetarajiwa kufundishwa katika viwango vyote viwili, kiwango cha kidato cha nne na cha sita zimependekezwa.

Hata hivyo, suala la fasihi simulizi linahitaji kushughulikiwa kwa kina zaidi, hasa upande wa utendaji wa kazi katika vipera tofauti tofauti. Pia, wanafunzi wanaweza kuingizwa mapema katika ukusanyaji wa hadithi, ngano, visasili, tarihi, hekaya na vitendawili nyanjani. Kwa kufanya hivyo, walimu watakuwa wanawaingiza na kuwaandaa katika utafiti wa fasihi simulizi katika sijku za baadaye.

Waaidha, utanzu, wa hadithi fupi umepuuzwa katika silabasi ya shule za upili kama Samwel (2012:72) anavyosema kuwa, "ufundishaji wa hadithi fupi za kiswahili miongoni mwa Waswahili haupewi kipaumbele. Nchini Tanzania, kwa mfano, wanafunzi wa sekondari hawafundishwi kabisa utanzu huu. Wanafunzi hao wanasoma riwaya, ushairi, tamthiliya na kidogo fasihi simulizi lakini hadithi fupi hazisomwi na wakati mwingine hazitajwi kabisa. Utanzu huu huanza kufundishwa katika vyuo vikuu". Kwa hali hii kuna haja ya kutilia maana ufundishaji wa Hadithi fupi kwa kuiorodhesha katika silabasi ya shule za upili katika siku zijazo.

Aidha, kwa ujumla, silabasi za Kiswahili katika viwango vyote huchukulia kuwa matakwa ya wanafunzi wote nchini yametiliwa maanani. Usawazishaji huu, kwa njia moja au nyingine, haufai kwa sababu wanafunzi hawa hukulia katika mazingira tofauti tofauti. Wanafunzi waliokulia katika maeneo ya vijijini ni tofauti na wale ambao wamezaliwa, kukulia na kusomea katika shule zilizo mjini. Silabasi huchukulia kuwa wanafunzi wa vijijini ni sawa na wale wa mijini, hali ambayo si sahihi.

Halikadhalika, mitihani ya mwisho hutungwa kwa usawa kwa wanafunzi wote kutoka mazingira au maeneo tofauti. Kwa jumla, mitihani hii inapotungwa, huchukuliwa kuwa mada zote ambazo zimependekezwa katika silabasi zimefundishwa kwa wanafunzi wote nchini, hali ambayo ni potoshi kabisa. Pia, huchukulia kuwa mbinu za ufundishaji na ujuzi wa walimu wa Kiswahili ni sawa, hali ambayo si kweli.

Waaidha, wakuzi wa silabasi huchukulia kuwa, nyenzo kama vitabu na zana zingine zinazotumika katika ufundishaji ni sawa. Shule nyingi, (katika maeneo ya vijijini, na hata mjini), zina upungufu wa zana hizi. Hivyo basi, huu ni udhaifu mkubwa ambao silabasi haijautolea ufumbuzi kamili na, kwa njia moja ua nyingine, hutinga utekelezaji wa mapendekezo ya silabasi katika viwango vyote viwili.

Fauka ya haya, Taasisi ya Elimu Tanzania imewafanya walimu kuzembea katika maanadalizi ya maazimio ya kazi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, majedwali wanayotarisha hudumaza ubunifu wa mwalimu katikia utayarishaji wa maazimio ya kazi ya somo la Kiswahili. Aidha, kielelezo cha maazimio ya kazi kinapaswa kuandaliwa kwa makini kwa kukwepa makosa kama vile namna ya kuandaa malengo mahsusi. Labda, kile ambacho Taasisi ya Elimu ingefanya ni kutoa mfano wa maazimio ya kazi katika mada moja tu, halafu mwalimu ashughulikie mada zilizobaki katika muhula mzima kibinafsi. Hali hii itamkuza mwalimu kitaaluma na kumfanya kuwa mbunifu zaidi. Kilicho muhimu ni kuorodhesha mada zinazopaswa kufunzwa katika kila kiwango na pia malengo mahususi ambayo mwalimu anahitajikakuyafikia.

Waaidha, mada pendekezwa katika kila kiwango zidhihirishwe kwa uwazi, ili zichangie kuimarisha mbalimbali za lugha ya Kiswahili. Kimsingi, stadi za lugha ni nne: kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Ili mwalimu aweze kukuza stadi hizi miongoni mwa wanafunzi wake, anawajibika kunadaaa masomo mbalimbali yatakayochangia kuimarisha stadi husika.

Ikiwa mwalimu hataongozwa na stadi mbalimbali za lugha katika maandalizi ya masomo mbalimbali, ufundishaji wake utakuwa na doa. Kilicho muhimu ni kuwa, mwalimu anapoandaa somo lake, ajiulize litachangia kuimarisha stadi gani ya lugha. Vivyo hivyo, upangaji wa mada mbalimbali katika muhtasari wa masomo unapaswa kuongezewa safu ya stadi mbalimbali za lugha, jambo ambalo halijazingatiwa katika muhtasari wa Kiswahili kwa shule za upili. Aidha, stadi ya kuandika haijatiliwa maanani na watunzi wa silabazi. Huenda udhaifu huu ndio unawafanya wanafunzi wengi hata na walimu kutomudu stadi ya kuandika.

## Uchambuzi wa Viambajengo vya silabisi

Mwalimu anapotangamana na silabasi kwa mara ya kwanza anahitaji kufahamu vipengele mbalimbali katika muhtasari wa kila kidato, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Kama tulivyotanguliza kusema, silabasi ina vipengele kadhaa. Ujuzi, malengo ya muda mrefu, mada kuu, mada tegemezi, malengo mahsusi, mbinu za kufundishia, zana zu vifaa, upimaji na vipindi. Mwalimu anastahili kuchambua vipengele hivi, kimoja baada ya kingine, na kuvielewa. Katika silabasi ya Kiswahili, kila kidato kimeshughulikiwa kivyake kulingana na kiwango cha uelewa wa kidato husika. Hii ni kwa sababu, uelwea wa wanafunzi wa kidato

cha kwanza na kidato cha nne sio sawa. Ujuzi katika vidato na viwango vyote hutofautiana.

### Uchambuzi wa ujuzi

Ujuzi ni kauli zinazodhihirisha maarifa anayotarajiwa kupata mwanafunzi baada ya kufundishwa kwa muda fulani katika kila kidato. Kabla ya mada zitakazoshughulikiwa katika kila kidato,m ujuzi hudhihirishwa kwa uwazi. Mwalimu anapaswa kufahamu kwamba, ujuzi katika kila kidato na kiwango hutofautiana. Kwa hali hii, anastahili kusoma na kufahamu fika ujuzi unaotarajiwa kupatikana na wanafunzio wa kila kidato.

### Uchambuzi wa malengo

Kulingana na kamusi kamili ya Kiswahili (2009), lengo ni nia au kusudi. Kwa hivyo, malengo ni matarajio yanayopaswa kuhdihirishwa na mwanafunzi baada ya kufundishwa kwa muda fulani. Malengo yanayojitokeza kabla ya maudhui ya silabasi, baada ya ujuzi. Mwalimu anatahadharishwa kutochanganya malengo ya jumla na malengo mahsusi. Lazima abainishe kwamba, malengo tunayozungumzia ni malengo ya jumla ambayo ni tofauti na malengo mahsusi yanayodhihirika katika andalio la somo. Kwa kawaida, malengo mahsusi yanapotarajiwa yafikiwe baada ya dakika arobaini. Mwalimu, anapaswa kufahamu kuwa malengo ya jumla sio lazima yawasilishwe kwa vitenzi dhhiri vinavyoweza kupimika, na kufikiwa kwake ni kwa muda mrefu.

### Uchambuzi wa Mada Kuu na Mada Tegemezi

Mada kuu, kwa kifupi, hutaja maudhui yatakayoshughulikiwa katika silabasi na kudhihirishwa kwa herufi kubwa. Mada tegemezi huzijenga mada kuu. Katika muhtasari wa Kiswahili kwa shule za upili, mada tegemezi zinadhihirishwa kwa herufi ndogo. Kimsingi, katika muhtasari wa Kiswahili kwa shule za upili, mada kuu na mada tegemezi zimepangwa kwa nama fulani ambayo inamfunga mwalimyu kiasi kwamba hawezi kubadilisha mfuatano huu. Hata hivyo, cha msingi ni mwalimu kujiuliza kama mada husika zinachangia kuimarisha stadi gani ya lugha, ili asiishie katika kuimarisha stadi moja kwa muda mrefu, huku akipuuza zingine.

Kwa hivyo, ingefaa zaidi kama stadi za lugha zingetumiwa kama kigezo muhimu katika upangajui wa mada mbalimbali. Mwalimu anapoandaa maazimio ya kazi, anastahili kuorodhesha mada mbalimbali kulingana na namna zinavyochangia kuimarisha stadi

mbalimbali za lugha. Pia, mwalimu angeongozwa na hali kwamba, katika kila juma anawajibika kuimarisha stadi zote za lugha (stadi ya kusikiliza, kuongea, kusomka nja kuandika). Mpangilio ungemwezesha mwalimu kusambaza mada ambazo angezifundisha katika muhula mzima, huku akizingatia stadi mbvalimbali za lugha.

## Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Kuteua Mada za Mazomo Katika Silabasi

Mwalimu huandaa mada za kufunza kutokana na suilabasi kwa kuzivunja mada katika viwango vidogo ili viweze kufunika kwa urahisi. Aweze kupanga mada kulingana na muda uliowekwa wa miohula mitatu kwa mwaka. Mambo haya huzingatiwa:

- Ikiwa mada zinaingiliana na malengo ya elimu.
- Kama mada zinafunzika na kueleweka na wanafunzi wa kiwango sawa.
- Ikiwa mada inaingiliana na mazingira ya wanafunzi.
- Kama mada inapanua na kyukuza uelewa wa mwanafunzi./
- Ikiwa mada inampa mwanafunzi nmotisha ya kuendelea kusoma na kufahamu mambo anuwai.
- Kama mada inamwezesha mwanafunzi kuelewa mambo kwa njia ya kawaida kutokana nay ale aliyojifunza hapo awali.

## Uchambuzi wa Malengo Mahsusi

Malengo mahususi ni shabaha ambazo mwalimu anatarajia kumtimizia mwanafunzi baada ya kuhitimisha uwasilishaji wa somo lake. Kama tulivyotanguliza kusema, mwalimu anastahili kutofautisha malengo ya kiujumla ambayo hufikiwa kwa muda mrefu na malengo mahsusi ambayo hufikiwa kwa muda mfupi. Mwalimu anahitaji kufahamu kuwa, malengo mahsusi ndiyo dira inayomwongoza kufikia hatima ya safari yake ya kufundisha somo husika. Bila shabah, mwalimu atayumbayumba darasabni bila mwelekeo na hatimaye kuwapotezea muda, na hata kuwapotosha wanafunzi wake.

## Uchambuzi wa Ukuzaji au Uwasilishaji wa Somo

Ukuzaji wa somo hudhuhirisha vitendo ambavyo huzingatiwa na mwalimu na wanafunzo wake katika mchakato mzima wa uwasilishaji wa somo. Mwalimu anatarajiwa kufasili sehemu hii

kwa makini zaidi kwa sababu ndiyo husheheni ukuzaji wa somo. Katika sehemu hii, mwalimu anatarajiwa kushirikisha na kuchanganya mbinu mbalimbali za ufundishaji ili kudumisha hamu ya wanafunzi kwa somo husika.

Baadhi ya mbinu ambazo mwalimu anaweza kushirikisaha katika ufunzaji wake ni pamoja na uulizaji na ujibuji maswali majadiliano, matumizi ya mifano, umotishaji na ubadilishaji hali.

Licha ya kuzingatia mbinu mbalimbali za ufundishaji, mwalimu anatarajiwa kushirikisha vifaa au zana alizokusudia kumsaidia katika ufundishaji wa somo.

## Uchambuzi wa Zana au Vifaa

Katika silabasi ya Kiswahili kwa shule za upili, zana ni muhimu katika mchakato mzima wa ufundishaji kwa sababu humsaidia mwalimu katika uwasilishaji wa somo lake ili aweze kufikia malengo mahsusi. Kama tulivyotangulia kusema, katika utoshelevu wa silabasi ya Kiswahili, upendekezaji wa zana humfanya mwalimu kuwa mzembe na kumdumaza kifikra kiasi kwamba hawezi kuwa mbunifu. Ingefaa mwalimu apewe fursa ya kubuni vifaa kna uelewa wa wanafunzi wake na mazingira yanayowazunguka. Pia, mwalimu anatarajiwa kuteua marejeleo yatakayomsaidia kufanikisha somo lake kulingana na uelewa wake na ule wa wanafunz wake. Hata hivyo, anashauriwa kuzingatia marejeleo ambayo yanaendana na kiwango cha wanafunzi wake na yaliyopendekezwa na Taasisi ya Elimu nchini Tanzania.

## Uchambuzi wa Upimaji

Upimaji ni sehemu muhimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji, kwani humfanya mwalimu kuwa tayari anapojiuliza maswali mbalimbali baada ya kila hatua katika uwasilishaji wa somo lake. Majibu ya maswali anayojiuliza katika kila hatua yanamkumbusha ikiwa malengo yake mahsusi yameshaafiwa au la. Maswali haya ni kigezo muhimu cha kumwezesha mwalimu aweze kujua iwapo shabaha zake mahsusi zimefikiwa au la.

### Uchambuzi wa Upimaji wa Kufaulu kwa Ufundishaji wa Mada Pendekezwa Katika Silabasi

Baada ya masomo mbalimbali kuwasilishwa kwa wanafunzi katika kila kidato, kuna haja ya kupima iwapo matokeo ya ujifunzaji yameafikiwa au la. Mwalimu anapotathmini wanafunzi wake, anaweza kufikia uamuzi wa kutathmini mbinu za ufundishaji, zna

anazozitumia ili kuboresha uelewa wa wanafunzi wake utendakazi wake. Upimaji unaweza kujitokeza kwa namna mbili, upimaji endelezi na upimaji wa mwisho wa muhula.

Katika **upimaji endelezi,** mwalimu anaweza kuwatathmini wanafunzi wake ama kwa kila juma au kila mwezi. Mijarabu mbalimbali inayoweza kupima stadi mbalimbali kama kusikiliza, kuongea, kusoma au kuandika, inaweza kuandaliwa ndani ya juma moja au mwezi. Kwa upande wa **mitihani,** mwalimu anaweza kuwatathmini wanafunzi wake katikati ya muhula na mwishio wa muhula na kuunganisha alama zote kwa pamoja, ili baadaye aziunganishe na aalama za upimaji endelezi, hizi zikiwa ni alama za mijarabu mbalimbali. Mwalimu anashauriwa kuwatathmini wanafunzi wake kila wakati.

## Uchambuzi wa Maazimio ya Kazi

Maazimio ya kazi humpatia mwalimu mwelekeo wa jinsi atakavyoshughulikia ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Aidha, hii ni dira inayomwongoza mwalimu katika safari ndefu ya kufikia malengo ya jumla na malengo mahsusi. Maazimio ya kazi husheheni sehemu mbili kuu: taarifa tangulizi na jedwali maalumu linalodhihirisha vipengele mbalimbali. Taarifa tangulizi hupambanua mwandalizi wa maazimio ya kazi, shule anayofundisha, kidato husika, muhula pamoja na mwaka anaotayarisha maazimio ya kazi. Taarifa kuhusu muhula na mwaka ni muhimu kwa sababu, humwondeshea mwalimu kishawishi cha kutumia maazimio ya kazi kwa mara ya pili mwaka unaofuatia.

Sehemu nyingine inayodhihirika katika taarifa tangulizi ni ujuzi ambao mwanafunzi anatarajiwa kupata. Walimu wanashauriwa kuzingatia ujuzi unaopendekezwa katika silabasi ili aweze kuwapatia wanafunzi wake maarifa yanayotarajiwa na yafaayo. Kimsingi, jedwali la maazimio ya kazi hubeba safu kadhaa huku ikitegemea eneo ambalo Kiswahili kinafundishwa. Katika kazi hii, safu zinazozingatiwa ni tisa (9); ambazo ni Juma, kipindi, stadi, mada kuu na mada tegemezi, malengo mahsusi, shughuli za mwalimu na mwanafunzi, nynzo, upimaji na maoni. Katika sur ifuatayo, yaani sura ya nne kila safu imefafanuliwa kwa mapana na marefu.

Aidha, safu ya stadi, ndio uti wa mgongo wa upangaji wa mada zinazokusudiwa kufundishwa katika muhula mzima, na hatimaye mwaka mzima katika kila kidato. Hii ni kwa sababu, ili mwalimu

ajiepushe na hali ya kusisitiza stadi moja na kupuuza zingine bila kujua, anahitaji kutilia maananio stadi zote za lugha. Mwalimu ana wajibu wa kuchambua na kuorodhesha mada zinzaoimarisha stadi mbalimbali. Kwa mfano, anapaswa kuorodhesha mada zinazoimarisha stadi ya kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Baada ya kuorodhesha mada husika, huku zikienda sambamba na stadi mbalimbali za lugha, atakapokuwa akiandaa maazimio na stadi mbalimbali za lugha, atakapokuwa akiandaa maazimio ya kazi inakuwa rahisi kwa mwalimu kusambaza mada mbalimbali katika kila juma kwani kila stadi ya lugha itaweza kuimarishwa.

## Uchambuzi wa Andalio la Somo

Katika sura ya nne, andalio la somo limeshughulikiwa kwa mapana zaidi. Kimsingi, andalio la somo lina sehemu nne muhimu ambazo ni sehemu ya taarifa tangulizi inayobeba taarifa kumhusu mwalimu, shule, kidato husika, somo, muhula, mwaka na jedwali linalodhihirisha, tarehe ya somo kufundishwa, kidato kitakachofundishwa, kipindi, muda utakaochukuliwa na somo husika na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa na idadi kamili itakayohududhuria kipindi husika.

Pia, katika taarifa awali, ujuzi ambao mwanafunzi anataamiwa kupata umedhihirishwa. Halikadhalika, stadi itakayoimarishwa na somo husika imedokezwa. Vivyo hivyo, lengo la kiujumla na malengo mahsusi ya somo yamepambanuliwa. Nyenzo na mbinu za kufundishia zimeainishwa pia.

Sehemu ambayo ni muhimu, na inahitaji uchambuzi ni sehemu ya ukuzaji wa somo. Katika utangulizi, mwalimu anahitajika kubuni utangulizi ambao utachochea fikra za wanafunzi ili uweze kuwamotisha na kuzua hamu miongoni mwao. Kwa upande wa uwasilishaji, mwalimu anahitajika kushirikisha mbinu kadhaa za ufundishaji ambao zitamotisha na kudumisha hamu ya wanafunzi waendelee kumsikiliza mwalimu badala ya kusinyikana kuanza kushiriki katika vitendo vilivyo nje ya somo. Mwalimu (katika hatua hii), anashauriwa kuwashirikisha wanafunzi wake ipasavyo ili kuwadhibiti katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

Baadaye, mwalimu anastahili kukadiria aliyoyawasilisha kupitiakuwauliza wanafunzi maswali; maswali ambayo yanaweza yakawa ya kimaongezi au kimaandishi, huku ikitegemea alikuwa akiimarisha stadi gani ya lugha. Kama utangulizi katika somo,

akiimarisha stadi gani ya lugha. Kama utangulizi katikasomo, hitimisho ni muhimu zaidi kwa sababu hukamilisha safari ndefu ya mwalimu katika uwasilishaji wa somo. Hivyo, katika hatua hii, mwalimu anapaswa kupima malengo mahsusi aliyojiwekea katika somo. Anapaswa kutoa muhtasari wa somo lake kwa njia ya maswali kimaongezi ili kukadiria iwapo shabaha zake zimefikiwa au la. Mwalimu anapaswa kujiuliza ili ajue shabaha zake zimefikiwa kwa kiwango gani kulingana na jinsi wanafunzi wake wanavyoyajibu maswali anayowauliza.

**Mpangilio wa ubao** ni muhimu kwa mwalimu kwa sababu humtayarisha kufikiria jinsi ambayo ubao wake utakavyokuwa katika somo halisi. Pia, mpangilio huu humwandalia mapema sehemu ambayo atawaandikia wanafunzi wake hoja muhimu, (na ambayo ni katikati ya ubao). Waaidha, mwalimu anahsauriwa kuandika mambo yasiyo muhimu katika sehemu ya kushoto ya ubao na chati yake aibandike katika sehemu ya kulia ya ubao.

Mwalimu anapofikia hatima ya somo lake, anatarajiwa kujitathmini, yaani kiwango ambacho wanafunzi wake wameelewa. Mwalimu anatahadharishwa kuwa, tatahmini yake isiwe ya kiujumla. Katika kujitathmini, mwalimu anatarajiwa kurejelea malengo mahsusi aliyojiwekea awali katika somo lake. Kwa mfano, ikiwa lengo mahsusi lilikuwa "Mnamo mwisho wa somo, kila mwanafunzi aweze kutaja walau vipera sita vya hadithi", mwalimu anatarajiwa kujitathmini hivi: "Lengo mahsusi la somo likifikiwa kwa sababu takriban wanafunzi asilimia 95 waliweza kutaja walau vipera sita vya hadithi." Walimu wanatahadharishwa kutojitathmini hivi: "Wanafunzi walielewa somo au wanafunzi walifurahia somo".

## Sifa za mwalimu wa Kiswahili

Kazi ya mwalimu ni kama safari ndefu, na huanzia anakokujua akielekea asikokujua. Safari hii inabidi ikamilishwe kwa uangalifu na utalaamu wa hali ya juu. Lazima tfahamu kwamba taaluma ya ualimu inafanana nay a nahodha wa mweli ambaye ana jukumu la kuongoza chombo hadi kifike mwisho wa safari bila ya ajali yoyote. Hivyo basi mwalimu wa kiswahili, kama alivyo nahodha wa mweli, anahitaji kuongoza wanafunzi wake darasani katika masomo mbalimbali ili asije akavuruga utaratibu wa masomo husika na kukwamisha juhudi za kufikia malengo yake. Lichaya kufundisha, mwalimu anahitaji kuwaongoza wanafunzi wake kinidhamu ili watakapohitimu wawe ni watu wa kutegemewa.

Baadhi ya sifa za mwalimu anayefaa kuitwa mwalimu wa Kiswahili katika shule za upili ni pamoja na:

**(a) Kuwa na ufahamu kabambe wa lugha ya Kiswahili**

Mwaklimu wa kiswahili, anatakuiwa kuwa na ufahamu unaozidi wanafunzi wake. Sarufi ya Kiswahili lazima aifahamu fika. Endapo atagundua baadhi ya wanafunzi ni magwiji wa lugha ya Kiswahili, atanahitajika kwenda hatua moja au mbili zaidi, hususani kuwa mgeni wa maktaba na kujifunza zaidi ili asije akadharauliwa na wanafunzi wake. Vilevile, ikiwa ana matatizo ya matamshi, anapokosea utamkaji wa baadhi ya sauti za lugha ya Kiswahili, anapaswa kujirekebisha papo kwa hapo. Anashauriwa kutoona haya anapojikosoa yeye mwenyewe kuliko kukosolewa na wanafunzi wake. Lazima tukubali kwamba, wazungumzaji wengi wa lugha ya Kiswahili sio wazawa asilia wa jamii ya waswahili na, kwa hali hii, wakati mwingine hujikuta wanaathiriwa na lugha mama. Mwalimu hapaswi kujimudu tu katika lugha ya Kiswahili, lakini anatarajiwa kuimarika zaidi kwa upande wa fasihiya Kiswahili. Ufahamu wa nadharia mbalimbali za uhakiki wa fasihi ni muhimu. Mwalimu wa fasihi ya Kiswahili, anapoanza kuzungumzia uchambuzi wa kazi za fasihi, atajikuta akizungumza nadharia (Khamisi, 2008)

**(b) Mwalimu kama kielelezo**

Mwalimu wa Kiswahili anahitajika kuwa kielelezo kwa wanafunzi, ndani na nje yadarasa. Wanafunzi wa shule za upili huwa hawajakomaa kabisa kiakili na kimwili na mara nyingi huiga wanayoyaona yakitendeka; yawe ni mavawi au tabia za waaalimu wao. Hivyo basi, mwalimu anahitaji kuwa mfano wa kuigwa na wanafunzi wake. Anayoyasema ana wajibu wa kuyakadiria na kuyapima kabla ya kuyasema; ndani au nje ya darasa.

**(c) Uchangamfu na bidii**

Taaluma ya ualimu tofauti na taaluma zingine, hususani uaskari huhitaji uchangamfu kwa kiasi fulani. Mwalimu ambaye ataingia darasani akiwa amevaa sura ya askari, huwa anatisha na kuwaogofya wanafunzi wake kiasi kwamba, usikilizaji na ufahamu wao unatingwa na haliu ya mwalimu wao. Kwa hali hii, mwalimu anapoingia darasani, anashauriwa kuwa mchangamfu na mcheshi kwa sababu hali hii itawafanya wanafunzi wake kuchangamka na kupokea anavyowafundisha bila kuogopa. Halikadhalika, mwalimu anapaswa kudhihirisha bidii kazini kwa kuhudhuria vipindi vyake

vyote na kutochelewa. Wanafunzi, bila shaka, wataiga yale ambayo yanafanywa na mwalimu wao. Kwa hali hii hawatachelewa kufika darasani na vilevile, watadhihirisha juhudi za kufanya kazi ya ziada waliyokuwa wamaeachiwa na mwalimu wao.

**(d) Uwajibikaji darasani**

Mwalimu anahitajika kuwajibika kwa kuwa macho zaidi, hasa kwa wanafunzi ambao ni watundu na wakorofi darasani. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao hawazingatii yale mwalimu anawaelekeza wafanye, ila huwabugudhi wenzao. Kwa mfano, wanafunzi wa kidato cha pili ambao huwa wanapitia katika mabadiliko ya kimaumbile, mara nyingi, huwatatiza waalimu ndipo sasa wanatahadharishwa kuwa macho zaidi kwao wakilinganishwa na wanafunzi wa vidato vingine. Ikiwa wanafunzi wataonesha utovu wa nidhamu, mwalimu anashauriwa kuwashughulikia papo kwa hapo na sio kusubiri.

**(e) Mwalimu kuwa nadhifu**

Waalimu wote, kwa jumla, wanashauriwa kuwa nadhifu. Mavazi yao yanahitajika kuwa safi na yaliyopigwa pasi. Mwalimu, pia anahitajika kunyolewa kwa kuzingatia mtindo ambao hautakuwa unakiuka maadili ya taaluma ya ualimu. Vivyo hivyo, ikiwa mwalimu ana mazoea ya kutonyoa, kuna haja ya kuchana nywele zake ipasavyo. Fauka ya haya, waalimu wa kike wanashauriwa kuvaa mavazi ambayo yanaendana na taaluma ya kazi yao. Mavazi ambayo yanatangaza sehemu ambazo hazipaswi kuonekana hadharani hayafai. Bila shaka, mavazi ya aina hii huwanjui heshima na huwafanya wanafunzi wao kuwadharau.

**(f) Uwasilishaji wa somo kwa njia ifaayo**

Mwalimu anapaswa kuwasilisha somo la Kiswahili kwa sauti ambayo ni ya wastani, na ambayo haitawabughudhi wanafunzi wake. Sauti ya chini huwafanya baadhi ya wanafunzi kutosikia mada inayowasilishwa na mwalimu. Kwa upande mwingine ikiwa sauti ya mwalimu itakuwa ni ya juu, bila shaka, itaathiri usikilizaji wa wanafunzi, kwani itageuka kuwa kelele.

**(g) Mwalimu kuwa mlizi wa muda wa kila kipindi**

Mwalimu anahimizwa kuzingatia muda aliotengewa katika ratiba ya mafunzo. Walimu, mara nyingi, wanakwaruzana na kutofautiana kwa sababu ya baadhi yao kutoheshimu muda waliotengewa. Mwalimu wa Kiswahili anahitaji kudumisha muda wa somo lake. Kwa kufanya hivyo, kunamwondoshea na kumwepushia migogoro

na migongano na walimu wa masomo mengine. Vilevile, wanafunzi hujifunza kutokana na vitendo vya walimu wao. Hivyo, wanafunzi kupitia kuiga mwalimu wao anayetunza muda, hata na wao watashawishika kufanya vivyo hivyo na baadaye kuwa watu wakutegemewa katika jamii.

**(h) Mwalimu kumakinika katika maandalizi**

Mwalimu ana wajibu wa kujiandaa kabla ya kuingia darasani. Maandalizi haya hayafanwi katika siku moja, ila huwa ni ya muda mrefu. Mosi, mwalimu wa Kiswahili anahitaji kutangamana na mtaala wa masomo ya Kiswahili na kuufasili. Pili, baada ya kutangamana na mtaala, mwalimyu anahitaji kuandaa maazimio ya kazi ambayo ndiyo dira itakayomwongoza katika muhula au mwaka mzima. Tatu, mwalimu atalazimika kuandaa masomo mbalimbali ya Kiswahili ili asije akawapotosha wanafunzi wake.

**(i) Mwalimu mwenye sifa botra huongozwa na shabaha za somo**

Mwalimu ambaye hana andalio la somo ni sawa na rubani au nahodha ambaye hana dira. Kwa hali hii, shabaha za somo lake darasani. Bila shabaha hizi, mwalimu ataishia kuwapotezea wanafunzi muda. Shabaha (ambazo ni malengo ya muda mfupi), zinamwongoza mwalimu katika safari yake ya ufundishaji.

**(j) Mwalimu bora huandaa nyenzo**

Nyenzo ni visaidizi vya mwalimu katika somo lake. Hivi ni vifaa ambavyo vinaweza kuwa ni halisi au ni vibadala. Kwa mkabala huu, mwalimu anapotayarisha maazimio ya kazi, anashauriwa kubainisha vifaa ambavyo atatumia katika kila somo. Ili wanafunzi waweze kuwa na uelewa kabambe, kila somo linahitaji kuwa na vifaa vyake; view ni halisi au vibadala. Kwa mfano, ikiwa mwalimu anataka kufundisha fasihi simulizi inayohusiana na ngoma ya wasukuma, vifaa haluisi vitakuwa ni vyombo kama njuga na ngoma. Iwapo vyombo hivi vitawasilishwa kwa michoro, basi michoro husika itachukua nafasi ya vifaa halisi.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, baada ya kukamilisha somo hili kuna haja ya kufanya tafakuri kuhusiana na yale uliyojifunza ili kuona kama somo letu limeeleweka.

## Zoezi la Somo

1. Fafanua kwa tafsili mambo ambayo ungezingatia katika uteuzi wa mada ambazo zinapaswa kuwekwa katika silabasi ya kiswahili.
2. Chambua kwa kina silabasi ya Kiswahili kwa kidato cha kwanza hadi cha nne.
3. "Stadi za lugha ni uti wa mgongo wa upangaji mada katika maazimio ya kazi". Jadili
4. Fafanua umuhimu wa mpangilio wa ubao katika mchakato wa ufundishaji.
5. Tathmini utoshelevu wa silabasi ya Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.
6. Fafanua maanaya dhana ya lugha kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali.
7. "Kwa mujibu wa sifa za lugha, lugha hujizalisha na kujinyumbulisha au hufa". Jadili kauli hii kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili.
8. "Mwalimu ndiye uti wa mgongo wa lugha ya Kiswahili".
9. "Lugha yoyote ina uwezo wa kuzalisha maneno au kufa". Jadili kauli hii kwa kutumia lugha ya kami.
10. Dadavua sifa faafu za mwalimu wa fasihi ya Kiswahili.

# Somo la Pili

## Maandalizi ya Mwalimu

### Utangulizi

Maandalizi ya mwalimu kabla ya kuingia darasani ni muhimu. Mwalimu anayejiandaa kuwa mwalimu kabla ya kuhitimu katika taaluma ya ualimu, lazima kwanza apitie katika mchakato wa kufanya maandalizi kabambe anapojiunga na chuo kikuu. Mwalimu ambaye hashiriki katika mazoezi ya nyanjani ni sawa na rubani ambaye hajapitia katika mafunzo ya urubani na anahitajika kuendesha ndege. Bila shaka, ikiwa ataruhusiwa kuendesha ndege husika, ataishia kusababisha ajali na kuwaua abiria wote. Vivyo hivyo, mwalimu ambaye hajajiandaa vya kutosha ataishia kuwapotosha wanafunzi wake, na kazi yake, kwa ujumla, itakuwa chapwa. Kwa mkabala huu, mwanafunzi anapojiunga na mafunzo na taaluma ya ualimu, anahitajika kutangamana na hati za taaluma ya ualimu. Hati hizi za taaluma ya ualimu ni pamoja na:

- Silabasi
- Maazizimio ya kazi
- Andalio la somo
- Kumbukumbu ya yalifundishwa na kumbukumbu ya tathmini endelezi

**Tanbihi:** Tutatumia Tanzania kama mfano wa kufafanulia nafasi ya hati za taaluma ya ualimu.

### Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

▪
▪
▪

### Silabasi

Silabasi ni muhtasari wa mada mbalimbali zinazonuiwa kufundishwa katika viwango tofauti vya elimu kwa muda fulani, muda ambao unaweza kuwa ni mwaka mmoja katika kila kiwango. Silabasi ni zao la mtaala wa elimu na huzalishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi. Hati ya muhtasari wa Kiswahili iliandaliwa kwa shule za upili mwaka wa 2005 kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, na kwa kidato cha tano hadi cha sita, mwaka wa 2009.

Muhtasari wenyewe hushehesni yafuatayo:

- Malengo ya elimu nchini Tanzania
- Madhumuni ya elimu atakaoputa mwanafunzi katika somo la Kiswahili
- Ujuzi wa jumla atakaoupata mwanafunzi katika somo la Kiswahili
- Malengo ya jumla ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili
- Mada zitakazofundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne
- Mbinu mbalimbali zinazotumiwa na mwalimu kufundishia mada mbalimbali
- Vifaa au zana mbalimbali zinazotumiwa kuhimili ufundishaji wa mada mbalimbali

**Umuhimu wa silabasi**

- Kudhibiti elimu inayotolewa katika shule zote za upili kwa kuhakikisha wanafunzi nchini wamepokea elimu sawa.
- Silabasi huorodhesha kwa njia zenye muwala kuanzia kwa mada sahili kuelekea kwenye mada tata.
- Silabasi uhakikisha mada zimeshughulikiwa kwa kuzingatia muhula na mwaka ambapo zitafundishwa.
- Silabasi hupanga mada kwa mantiki fulani, huku zikitegemeana, hatua kwa hatua. Mada moja lazima ifundishwe kabla ya nyingine.
- Silabasi huhakikisha kuwa kinachopendekezwa kufundishwa katika kiwango fulani kinatekelezeka na kufikiwa kulingana na uwezo wa wanafunzi.
- Silabisi huhakikisha kuwa kinachopendekezwa kiufundishwa katika kiwango fulani kinatekelezeka na kufikiwa kulingana na uwezo wa wanafunzi.
- Silabasi huhakikisha kuwa malengo ya somo la Kiswahili yanaongoza na kuelekeza mbinu za ufundishaji ambazo mwalimu anapaswa kuzingatia anapofundisha mada fulani.

- Kumsaidia mwalimu kuandaa maazimio ya kazi.

## Udhaifu wa Silabasi

- Haitilii maanani mahitaji ya kila mwanafunzi-wanafunzi wanaotoka katika mazingira tofauti na kuwafunza mambo sawa, hutakidhi mahitaji yao kimazingira.
- Mitihani inayotungwa ghuwa ni sawa na inachukuliwa kuwa mada zote zimefunzwa kwa kutumia njia za kufundishia ambazo ni sawa, waalimu wote wana tajiriba sawa na vifaa vya kufundishia ni sawa. Matokeo ni kuwa, shule ambazo zina walimu na vifaa vya kutosha hupata matokeo bora kuliko shule zisizokuwa na walimu wa kutosha wala vifaa.
- Mada nyingi ni pana na muda wa kuzishughulikia ni mdogo.
- Silabasi haitilii maanani muda wa shughuli nyinginezo shuleni kama vile michezo na mihadhara ya wageni.
- Silabasi aghalabu imetungwa kinadharaia na wala si kiutendaji. Hutegemea ujuzi wa mwalimu katika kuvunjavunja mada husika katika vipengele rahisi na vinavyofunzika.

## Maazimio ya Kazi


Maazimio ya kazi ni mpango wa kazi au mada zitakazofundishwa katika muhula au mwaka mzima. Hati hii humpa mwalimu fursa ya kupanga atakavyoyafundisha ili yawe na utaratibu fulani na yaweze kufikiwa kwa muda uliowekwa. Maazimio ya kazi ni muhimu katika ufundishaji wa somo lolote. Hii ni kwa sababu, mwalimu ambaye anathamini na kuipenda kazi yake, ni lazima aandae hati ya maazimio ya kazi bila kushurutishwa na yeyote. Ni wazi kuwa, mwalimu anayekosa hati hii ni sawa na nahodha wa meli anayekosa dira katika uendeshaji wa chombo chake. Bila shaka, matokeo ya safari yake hayawezi kuwa ya kuwaridhisha abiria wake, kwa sababu itakuwa ni bahati kama hata sababisha ajali. Vivyo hivyo, kwa mwalimu aliyekosa kuwa na maazimio ya kazi, hupoteza mwelekeo katika taaluma yake na matokeo ya upungufu huu, ni kutofautisha wanafunzi katika mitihani yao. Maazimio ya kazi ni zao la muhtasari wa mafunzo au silabasi ambayo chimbuko lake ni malengo ya elimu ya taifa. Kabla ya mwalimu kuazimia

kuandaa maazimio ya kazi, anawajibila kuhakikisha kuwa ana vianzo vya kutosha. Malighafi anayohitaji katika utayarishaji wa maazimio ya kazi ni:

- Silabasi
- Vitabu vya wanafunzi
- Miongozo na vitabu vya marejeleo ya mwalimu
- Vitabu vya ziada au kiada
- Ratiba ya masomo

**Tanbihi**

Uhusiano kati ya mahitaji haya ya msingi unaoweza kurodheshwa kupitia kielelezo hiki:




**Sifa za maazimio ya kazi mwafaka**

- Lazima yaandaliwe kutokana na muhtasasari wa mafunzo
- Yawe mafupi na yenye kueleweka
- Yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya kitaaluma
- Sharti yadhihirishwe mtiririko au muumano wa mada kuu au mada tegemezi
- Yadhihirishe safu za shabaha, mada kuu, mada tegemezi, shughuli za mwalimu na mwanafunzi, nyenzo, tathmini na maoni.
- Pia, yanapaswa kudhihirishwa kwa uwazi taarifa tangulizi (jina la mwalimu, jina la shule, muhula, mwaka wa kuandaa maazimio ya kazi, jina la somo na kidato husika).

**Muundo wa maazimio ya kazi**

Maazimio ya kazi huwa na sehemu kuu mbili:

a) Sehemu ya taarifa tangulizi

b) Vijenzi vya maazimio ya kazi

**Sehemu ya taarifa awali au jalada**

Sehemu ya taarifa tangulizi inajumlisha

- Jina la mwanadalizi wa maazimio ya kazi
- Jina la shule
- Muhula ambao maazimio ya kazi yatatumika
- Mwaka ambao maazimio ya kazi yatatumika
- Jina la somo
- Kidato ambacho maazimio ya kazi yameandaliwa
- Ujuzi.

**Vijenzi vya maazimio ya kazi**

Sehemu hii ya maazimio ya kazi ina vijenzi kumi na viwili:

Sehemu hii ya maazimio ya kazi ina vijenzi kumi na viwili:

- Juma
- Kipindi
- Funzo
- Mada kuu
- Mada tegemezi
- Mbinu za kufundishia
- Shabaha
- Shughuli za mwalimu na mwanafunzi
- Nyenzo (maraejeo na vifaa au zana) na
- Mazoezi
- Maoni

**Juma**

Kijenzi hiki huonyesha jumla ya majuma katika muhula au mwaka mzima. Kuna haja ya mwalimu kushughulikia takriban kila stadi ya lugha katika kila juma.

**Kipindi**

Safu ya kipindi katika maazimio ya kazi hudhihirishaidadi ya vipindi kwa somo katika juma nzima, kimsingi, kulingana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, vipindi vya Kiswahili katika kila kidato ni vitatu (3) katika shule za upili, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Katika kipindi cha kwanza, cha pili na cha tatu, mwalimu anapaswa kuzingatia mada zinazoimarishastadi ya kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika mtawalia.

**Stadi**

Safu hii hupambanua stadi za lugha ambazo ni kusikiliza, kuongea, kusoma a kuandika. Stadi za kusikiliza na kuongea huenda sambamba na kuzitenganisha na vigumu. Hivyo basi, mwalimu anapotayarisha maazimio ya kazi anapaswa kuongozwa na safu ya stadi. Mwalimu anapoandaa somo lolote, anapaswa kujiuliza funzo lenyewe litaimarisha stadi gani ya lugha. Safu hii ndio hutofautisha somo la lugha na masomo mengine. Kwa bahati mbaya kielelezo cha maazimio ya kazi kilichotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hakibainishi safu hii.

**Mada kuu**

Safu ya mada kuu hupambanua mada muhimu itakayoshughulikiwa. Kwa mfano, "Aina za maneno" inaweza kuwa mada kuu hali mada tegemezi ikawa "majina", "vivumishi" au "vitenzi".

**Mada tegemezi**

Safu ya mada tegemezi hupambaua mawanda maalumu yatakayoshughulikiwa au yatakayofundishwa. Mfano unaorejelewa hapo juu unaweza kuafiki mada tegemezi. Katika silabasi tunayoirejelea, madakuu a mada tegemezi hutokea katika safu

moja. Hata hivyo, mada kuu hudhihirishwa kwa herufi kubwa, hali mada tegemzi hupambanuliwa kwa herufi ndogo.

**Mbinu za kufundishia**

Safu hii hupambanua mbinu mbalimbali ambazo mwalimu anaweza kutumia ili kufaulisha somo lake. Kwa mfano, mbinu ya maswali na majibu, mjdala, mhadhara, matumizi ya mifano, umotishaji na mbinu ya kufunga na kufungua n.k.

**Shabaha**

Shabaha ni lengo mahususi la somo na hunuiwa kufikiwa baada ya kipindi kimoja. Shabaha huwa mwongozo wa kimsingi way ale ambayo yatashughulikiwa na mwalimu katika kipindi husika.

Shabaha inapaswa kutimiza matakwa yafuatayo:

- Iwe na uwezo wa kupimika
- Imlenge mwanafunzi sio wanafunzi
- Imlenge mwanafunzi na wala si mwalimu
- Ilenge mada funzwa
- Iwe na uwezo wa kutekelezeka
- Ibuniwe kwa vitenzi dhahiri au wazi. Kwa mfano “kujibu maswali, kutunga sentensi, kuandika maneno, kutamka sauti”. Vitenzi vifuatavyo ni mfano wa vitenzi ambavyo si dhahiri: kufahamu, kujua, kufurahia, kuelewa, kujibidiisha n.k
- Sahaba isugubikwe kwa maneno mengi.
- Shabaha ibainishe muda wa kutekelezwa
- Matokeo ya shabaha yanahitajika kudhihirika
- Ikawa shabaha ni zaidi ya mojalazima ziorodheshwe, (kwa hakika hakuna kipindi chenye shababa moja).

Kwa ujumla, shabaha zinapswa unadaliwa kwa kuzingatia kanuni ya MPAMU, kwa maana ya :

* M = Imlenge <u>M</u>wanafunzi

= Iwe <u>M</u>ahususi

* P = I<u>P</u>imike,

*   A  =  IAfikie

*   M  =  Iwe ndani ya Muda Maalumu

Shabaha zifuatazo zinaweza kuwa kielelezo cha shabaha mwafaka

- Kufikia mwisho wa somo kila mwanafunzi aweze
- Kueleza walau matumizi sita ya vyombo vya baharini
- Kutunga angalau sentenzi akizingatia msamiati mpya katika kifungu cha maneno
- Kujibu maswali yasiyopungua matano baada ya kusoma kifungu cha maneno “manufaa ya mnazi”
- Kutunga na kuandika walau sentensi tisa akizingatia msamiati wa maneno yanayokanganya.

**Umuhimu wa Shabaha**

- Huonyesha umuhimu wa somo kwa wanafunzi
- Hudhirisha tabia ya mwanafunzi baada ya somo
- Hufanya kazi ya mwalimu kuwa na maana
- Humwezesha mwalimu kufundisha kwa urahisi
- Humwezesha mwalimu kuzingatia mambo muhimu na kujiepusha kuenda nje ya mada.

**Shughuli za mwalimu na mwanafunzi**

Shughuli za mwalimu ni mambo yote yanayotekelezwa ama na mwalimu au mwanafunzi kabla ya kuingia darasani, na huwa yanafanywa hatua kwa hatua ili kufaulisha shabaha zilizobuniwa na mwalimu. Shughuli za mwalimu ni pamoja na kusoma marejeleo mbalimbali, kuandaa nukuu za kufundishia, kuandaa zana za kufundishia, kutalii maeneo yenye taarifa kuhusu mada husika, kuandaa na kuwapa wanafunzi maswali, na kuandaa somo kwa kutumia kinuruweo. Halikadhalika, shughuli za wanafunzi ni kama vile kusoma mapema kuhusu mada husika, kufanya masahihisho ya mada awali, kutafuta majibu kwa maswali yaliyotolewa na mwalimu, kuandaa mawasilisho, kujadiliana katika vikundi na kuandaa zana za kutumiwa katika kujibu maswali husika. Shughuli za mwalimu na mwanafunzi znapendekezwa kutokuwa chini ya nne, kwa kila muhusika. Aidha, shughuli za mwalimu huenda

sambamba naza mwanafunzi. Kwa mfano, iwapo mada kuu ni "ushairi" na mada tegemezi ni "uigizaji wa ngonjera", shughuli hizi zinaweza kuwa:

**Shughuli za mwalimu**

- Kusoma vianzo mbalimbali kuhusu ngonjera
- Kuandaa nukuu za kufudishia
- Kuchagua mashairi, (ngonjera) yatakayotumiwa darasani
- Kuandaa maswali yanayoruhusu ujibizanaji wa vikundi
- Kuwapa wanafunzi maswali ya vikundi
- Kuandaa andalio la somo

**Shughuli za mwanafunzi**

- Kusoma vianzo mbalimbali kuhusu ngonjera
- Kubainisha sehemu tata zinazohitaji ufafanuzi wa mwalimu
- Kujibu maswali katika vikundi
- Kujiandaa kwa mawasilisho kupitia ujibizaji katika kukariri ngonjera.
- Kugawana sehemu mbalimbali za uwasilishaji wa maswali.

**Nyenzo**

Nyenzo ni visaidizi vinavyomwezesha mwalimu kufundisha kwa urahisi na vizuri zaidi ili kufaulisha somo lake. Nyenzo zinaweza kugawika katika mafungu mawili

**a) Marejeleo**

Marejeleo ni vitabu, majarida au miognozo inayorejelewa na mwalimu katika utayarishaji wa maazimio ya kazi na pia kufundishia. Marejeleo hudhihirisha mwanadishi wa kitabu au jarida, mwaka wa uchapishaji, anwani ya kitabu (huandikwa kwa mlazo au kupigiwa mstari ikiwa kitabu kimechapishwa), mji ambapo kitabu kimechapishwa na shirika la uchapishaji. Kwa mfano

Wanjala, F. S (2011) Kitovu cha Fasihi Simulizi. Mwanza'; Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Kavoi, J. M. (1996) "Muwala wa Vipengele vya Fani: Uhakiki wa Kazi za Said Ahmed Mohamed" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro.

**Tanbihi**

- Anwani ya mswada (mfano wa pili) haijaandikwa kwa mlazo au kupigiwa mstari kwa sababu haujachapishw. Kimsingi, inapaswa kufungiwa katika alama za mtajo.
- Rejelea sehemu ya kwanza, sura ya pili kwa maelezo zaidi kuhusu mitindo ya upangaji wa marejeleo.

**b) Vifaa**

Vifaa ni zana mbalimbali ambazo mwalimu hutumia ili kuwasilisha na kufaulisha funzo lake kwa wanafunzi wake. Vifaa ni muhimu kwa sababu, huwafanya wanafunzi kuelewa kwa urahisi na kwa haraka tofauti na ikiwa mwalimu havitumii. Vifaa vinaweza kuainishwa katika mafungu mawili makuu.

**Vifaa halisi:** Hizi ni zana ambazo zi katika maumbile halisi na hazijabadilishwa kwa vyovyote vile. Ni vitu ambavyo vinaweza kubebwa hadi darasani. Kwa mfano, matunda, vyombo vya kupakulia chakula, mavazi mbalimbali n.k.

**Vifaa vibadala:** Vifaa vya aina hii huchukua nafasi ya vifaa halisi na ambavyo haviwezi kubebwa darasani. Vifaa hivi vinaweza kuwasilishwa kwa michoro, picha, chati, sanamu na vinyago.

**Sifa za vifaa mwafaka**

- Kifaa kiwe na umuhimu na chenye maana katika kufundisha yaani, kisalie kuwasilishamaana iliyokusudiwa.
- Kifaa kisiwe na habari au taarifa ya ziada isiyohitajika katika somo husika.
- Kifaa kisiwe na makosa ya hijai au upotofu wa taarifa iliyomo.
- Kifaa kiweze kuvuta nadhari ya mwanafunzi, yaani kiwe na haiba nzuri.

- Ubunaji wa vifaa utilie maanani mazgingira ya mwanafunzi.
- Kifaa kinachobuniwa na kutumiwa darasani kimsababishie mwanafunzi madhara yoyote.
- Vifaa view na uwezo wa kuhifadhika.
- Vifaa vinavyobuniwa vitilie maanani gharama ya utengenezaji

**Manufaa ya vifaa**

- Vifaa hurahisisha maelezo ya mwalimu
- Huokoa muda wa kuelezea mambo
- Vifaa huleta uwazi katika somo
- Vifaa humsaidia mwanafunzi kuelewa vizuri zaidi.
- Vifaa hupitisha maarifa kwa wanafunzi kwa urahisi
- Vifaa hukuza kipawa cha kuhifadhi mambo-wanafunzi hukumbuka walichofunzwa kwa urahisi.
- Ikiwa vina haiba nzuri, bila shaka, huwafurahisha na kuwachangamsha wanafunzi wakati wa kuwasilisha somo.
- Wanafunzi kupitia matumizi ya vifaa hujifunza utendaji zaidi ya kusikiliza.

**Tanbihi:** Ikumbukwe kuwa, sio kila somo linaweza kuandaliwa zana, aidha, mwalimu anapaswa kutundika zana yake wakati mwafaka tu ili zana isiwe chanzo cha kuwakanganya wanafunzi.

**Upimaji**

Safu ya upimaji hupambanua maswali ambayo mwalimu hujiuliza ili kukadiria kiwango cha uelewa wa wanafunzi baada ya kila hatua ya somo. Hii ni njia kabambe ya mwalimu kujitathmini na kukadiria iwapo wanafunzi wake walielewa alichokifundisha au la. Upimaji ni muhimu kwa sababu, huwa ni mizani kwa mwalimu kufanya maamuzi juu ya ikiwa atarudia hatua fulani kwanza, kabla ya kuendelea na hatua inayofuata. Aidha, kupitia usaidizi wa upimaji, mwalimu ataweza kuamua ikiwa baadhi ya wanafunzi wanahitaji mafunzo za ziadaau la. Mifano ya sentensi ya jinsi upimaji unapaswa kuendeshwa imetolewa katika kielelezo cha maazimio ya kazi katika safu ya upimaji.

**Manufaa ya Upimaji**

- Kupima uwezo wa mwnafunzi na kuelewa aliyofundishwa
- Kupima shabaha za mwalimu alizojiwekea mwanzoni mwa somo.
- Humwezesha mwalimu kufikia uamuzi ikiwa baadhi ya wanafunzi wanahitaji usaidizi.

**Maoni**

Safu ya maoni hudhihirisha kiwango cha uelewa wa wanafunzi baada ya somo. Pia, huonyesha kama somo limefundishwa au la. Ikiwa mwalimu hakufundisha, anahitaji kuelezea ni kwa nini na jinsi atakavyofidia kipindi husika. Fauka ya haya, ikiwa baadhi ya wanafunzi hawakuelewa kikamilifu, mwalimu anawajibika kuelezea katika safu ya maoni, na jinsi atakavyoshughulikia upungufu husika. Yanayopambanuliwa katika safu hii ni matokeo ya shabaha ambazo mwalimu alikuwa amejiwekea awali. Mwalimu anatahadharishwa kujitenga na maoni ya kiujumla kama "wanafunzi walielewa au lilikuwa somo zuri". Maoni yanapaswa kuwa maalumu, hususan "Asilimia 70 ya wanafunzi waliweza kutunga sentensi wakizingatia vitate" na asilimia 30 walishindwa. Kwa hivyo, nitatafuta wakati mwafaka wa kupitia mada husika pamoja na wanafunzi walioonyesha dalili za kutolewa. Safu hii hujazwa baada ya somo kukamilika.

**Manufaa ya maoni**

- Hudhihirisha iwapo kipindi fulani hakikushughulikiwa, na kwa nini, na jinsi mwalimu atakavyokifidia.
- Huonyesha kumbukumbu ya yaliyofundishwa na mwalimu.
- Humsaidia mwalimu mgeni kufahamu mwalimu aliyechukua nafasi yake alikofika.
- Huonyesha sababu za kutofundisha ikiwa kipindi husika hakikufundishwa.
- Huwa ni idhibati tosha kuwa mwalimu anafanya kazi ikiwa kutakuwa na kisingizio chake cha kutifanya kazi.

**Kielelezo cha Maazimio ya kazi**

**Jina la mwalimu:** Kazungu Katana

**Somo:** Kiswahili

**Jina la shule:** Luchelele

**Muhula:** I

**Kidato:** I

**Mwaka:** 2013

| Juma | Kipindi | Stadi | Mada Kuu/Mada Tegemezi | Malengo Mahsusi/ Shabaha | Shughuli za Mwalimu na Mwanafunzi | Nyenzo | Upimaji | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | Kusikiliza na kuongea | Hadithi | Mnamo mwisho wa kipindi mwanafunzi aweze; kutaja vipera vya hadithi kusimulia hadithi mbalimbali. | MWALIMU Kusoma kuhusu vipera vya hadithi. Kuandaa nukuu kuhusu vipera hadithi. Kuandaa hadithi moja ya kusimuliwa darasani. Kuwapa wanafunzi kazi ya vikundi kuhusu vipera vya hadithi. MWANAFUNZI Kusoma kuhusu vipera vya hadithi. Kutafutahadithi | Asilia Samwel, M (2012) Hadithi Fupi: Nadharia Mbibnu na mifano. Iringa: Kasenyenda Tanzania UK 19 Vifaa/zana Kanda za Sauti Video Zenye Hadithi | Je, mwanafunzi ameweza kuainisha viperavya hadithi na kuzifafanua? Je, mwanafunzi ameweza kusimulia hadithi? | |

| Juma | Kipindi | Stadi | Mada Kuu/Mada Tegemezi | Malengo Mahsusi/ Shabaha | Shughuli za Mwalimu na Mwanafunzi | Nyenzo | Upimaji | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kutoka kwenye makabala yao. | | | |
| | 2 | Kusoma | KUSOMA kwa ufahamu "Manufaa ya mnazi" | Mnamo mwisho wa somo mwanafunzi aweze: Kutunga sentensi akizingatia msamiati mpya katika kifungu "Manufaa ya mnazi", kujibu maswali baada ya kusoma | MWALIMU Kusomaufahamu mbalimbali. Kuchagua ufahamu mmoja kwa ajili ya somo husika. Kusoma ufahamu husika kwa makini huku akibainisha fani, maudhui na mafunzo. | Asilia Yahya J. na Khamai, K (1984) Kiswahili kwa Shule za Sekondari Nairobi: Longman. U.K 20 Vifaa Picha ya mti wa mnazi | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali baada ya kusoma kifungu cha maneno? | |

| **Juma** | **Kipindi** | **Stadi** | **Mada Kuu/Mada Tegemezi** | **Malengo Mahsusi/ Shabaha** | **Shughuli za Mwalimu na Mwanafunzi** | **Nyenzo** | **Upimaji** | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kifungu “manufaa ya mnazi | | | | |
| | | | | | MWANAFUNZI Kusoma ufahamu mbalimbali. Kujaribu kujibu maswali baada ya kila ufahamu. Kutafuta maana na matumizi ya misamiati mbalimbali kwa kutumia kamusi. | | | |
| | 3 | Kuandika | INSHA Hadithi ya kubuni | Mnamo mwisho wa somo mwanafunzi aweze: kutaja sehemu muhimu | MWALIMU Kurejelea vianzo mbalimbali kuhusu utungaji. Kuandaa nukuu kuhususifa za insha ya kubuni. Kuandaa kisa kimoja kama | Asilia Chesele, M (2021) Stadi za Uandishi wa Insha uk 40. **Vifaa** Chati yenye kielelezo cha | Je, mwanafunzi mewezakutaja sehemu muhimu za hadithi ya kubuni na kuandika? | |

| Juma | Kipindi | Stadi | Mada Kuu/Mada Tegemezi | Malengo Mahsusi/ Shabaha | Shughuli za Mwalimu na Mwanafunzi | Nyenzo | Upimaji | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | na kuandika hadithi ya kubuni kwa misingi ya fasihi simulizi. | insha kielelezo MWANAFUNZI Kusoma marejeleo mbalimbali kuhusu tungo. Kubainisha sehemu tata zinazohitaji maelekezo ya mwalimu. Kuandika kisa kama mfano wa insha. | hadithi ya kubuni | | |

**Manufaa ya Maazimio ya kazi**

- Humwezesha mwalimu kuhitimisha kazi kwa wakati na kukadiria muda unaohitajika.
- Humwezesha mwalimu kuandaa anadalio la somo.
- Humwezesha mwalimu kutambua vifaa vinavyohitajika na kujiweka tayari mapema, na panapo haja kutoa taarifakwa mwalimu mkuu ili vifaa vinunuliwe au kutolewa ghalani kwa wakati unaofaa.
- Humpa mwalimu nafasi ya kufikiria na kutafuta vitabu vya marejeleo kwa wakati unaofaa.
- Kwa kuzingatia malengo mahsusi au shabaha, mwalimu huweza kutunga mazoezi au majaribio mapema.
- Kwa kuzingatia shabaha, mwalimu huweza kutunga au kuandaa mtihani. Kwa kufanya hivyo mapema, huwa ana wakati wa kutathmini na kujua ikiwa unafaa kwa wanafunzi wake.
- Humsaidia mwalimu mgeni kujua mtangulizi wake alikokomea.
- Humpa mwalimu nafasi ya kuwaza juu ya mbinu za kufundishia na kuchagua zilizo bora.
- Maazimio ya kazi mazuri humfanya mwalimu kujiamini kufurahia, kupenda na kufanya kazi yake.
- Huwa ni dira wka mwalimu kwani humweongoza jinsi anapaswa kufuatanisha masomo yake kwa muhula au kipindi fulani.
- Ni kigezo tosha cha kupima jinsi mwalimu anavyoendeleakiwakati.
- Huondosha uwezekano wa mwalimu kurudia aliyokuwaamefundisha na kuwapotezea wanafunzi wake muda.

**Wakati Ufaao wa Kuandaa Maazimio ya Kazi**

Maazimio ya kazi yanapaswa kuandaliwa wakati wa likizo kwa sababu, shule zinapofunguliwa walimu huwa na kazi mbalimbali za kutekeleza hususani, kufundisha, kusahihisha na kujiandaa kwa michezo mbalimbali au drama n.k.

**Andalio la somo**

Andalio la somo ni mpangilio wa kina way ale mwalimu atakayofundisha, hatua kwa hatua, katika kipindi fulani. Hii ni hati muhimu katika taaluma ya ualimu, kwa sababu huwa kama dira ya kumwongoza mwalimu katika kipindi maalum ambacho huchukua muda wa dakika arobaini au dakika themanini (kipindi pacha) katika shule za upili. Hivyo basi, mwalimu anahitajika kuwaamejiandaa kabla ya kuingia darsani ili kujiepusha na hali ya kuwaharibia wanafunzi muda, au kujiaibishambele ya wanafunzi wake, endapo kwa bahati mbaya atakaukiwa au ataishiwa cha kuwafundisha.

**Sehemu za Andalio la Somo**

Andalio la somo linaweza kugawanywa katika sehemu nne:

- Taarifa tangulizi,
- Uendelezaji wa somo au ukuzaji wa somo,
- Mpangilio wa ubao
- Tathmini

**Sehemu ya Taarifa Awali**

Sehemu hii ni utangulizi katika andalio la somo na hudhihirisha jedwali ambalo huonyesha jina la somo, kipindi, tarehe, muda au wakati, kidato, idadi ya wanafunzi (iliyodahiliwa na iliyohudhuria). Baada ya kushughulikia jdwali lenye taarifa awali, habari zaidi hudhihirishwa kuhusu somo; nayo ni ujuzi, stadi, mada kuu, mada tegemezi (malengo) ya kiujumla, malengo mahsusi au shabaha nyenzo (vifaa au zana na marejeleo) na mbinu za kufundishia.

**Ukuzaji wa somo**

Sehemu hii hudhihirisha hatua mbalimbali ambazo mwalimu atawapitisha wanafunzi wake katika somo zima kuanzia utangulizi hadi hitimisho. Ukuzaji wa somo hudhihirisha hatua za utangulizi, uwasilishaji wa maarifa mapywa, ukadiriaji au uimarishaji wa maarifa mapya, upimaji na hitimisho.

Katika **utangulizi**, mwalimu anapaswa kuwaingiza wanafunzi wake katika somo. Utangulizi unahitajika kuzua hamu ya wanafunzi na, wakati huohuo, kuchochea fikra zao, ili uwashawishi kufikiri kuhusu mada husika. Utangulizi unahitaji kuunganisha mada awali na mada husika.

Katika sehemu ya **uwasilishaji,** mwalimu anatarajiwa kuwasilisha maarifa mapya jkwa wanafunzi, huku akizingatia mbinu mbalimbali. Baadaye, anahitajika kuimarisha maarifa mapya aliyoyawasilisha kwa mazoezi ya kutosha. Upimaji unamhitaji mwalimu kukadiria iwapo wanafunzi wake wanamweewa kabla ya kuendelea na hatua inayofuata. Waaidha, **hitimisho** ni muhimu katikakilasomo. Mwalimu, anatarajiwa kuhitimisha somo lake, huku akiongozwa na shabaha za somo. Anahitajika kuwauliza maswali yanayolenga kupima shabaha au malengo mahsusi aliyojiwekea.

Kimsingi, katika sehemu hii ya ukuzaji wa somo, kila hatua lazima ibainishwe itachukua muda gani. Aidha, kila hatua lazima idhihirishe shughuli za ufundishaji na shughuli za ujifunzaji, huku vikienda sambamba na ukadiriaji wa uelewa wa wanafunzi wake. Mwalimu anashauriwa kubainishwa mbinu za ufundishaji atakazotumia.

**Kielelezo cha Andalio la Somo**

**Jina la wmalimu:** Kazungu Katana

**Somo:** Kiswahili

**Jina la shule:** Luchelele

**Muhula:** I

**Kidato:** I

**Mwaka:** 2013

| Tarehe | Kidato | Kipindi | Muda | Idadi ya wanafunzi | |
|---|---|---|---|---|---|
| 05/01/2013 | 1 | 1 | 2:00 asubuhi | Iliyodahiliwa | Iliyopo |
| | | | | 45 | 43 |

**Ujuzi:** Kubainisha, kuhakiki na kutunga kazi za Fasihi Simulizi

**Stadi:** Kusikiliza na kuongea

**Mada kuu:** Fasihi Simulizi

**Mada tegemezi:** Hadithi

**Lengo kuu:** Kubainisha, kuhakiki na kutunga kazi za fasihi simulizi kwa Kiswahili

**Shabaha:** (i) Kutaja vipera kumi vya hadithi

(ii) Kufafanua viperakumi vya hadithi na

(iii) Kusimulia walau hadithi mbili

**Nyenzo: Marejeleo:** Samwel, M. (2012) *Hadithi Fupi: Nadharia Mbinu na Mifano*. Iringa: Kasenyenda Tanzania. Uk 19-21.

**Vifaa au Zana:** Kanda za sauti na video zenye hadithi

**Mbinu za kufundishia:** Mhadhara, maswali na majibu, matumizi ya mfano, kuiga na kuigiza na kuonyesha wazi.

**Ukuzaji wa somo**

| **Hatua** | **Muda** | **Shughuli za Ufundishaji** | **Shughuli za Ujifunzaji** | **Upimaji** |
|---|---|---|---|---|
| Utangulizi | 3 | *Mwalimu kuwauliza wanafunzi kutegeana vitendawili ili kuwaigiza katika funzo | *Kutegean vitendawili | Je, wanafunzi wameweza kutegeana vitendawili? |
| Uwasilishaji | 18 | *Mwalimu kuwauliza wanafunzi wataje aina za hadithi wazijuazo.<br>*Mwalimu kufafanua istilahi "hadithi".<br>*Mwalimu kusimulia hadithi moja kwa mfano.<br>*Mwalimu kutoa mifano zaidi ya hadithi kupitia kanda za sauti na kuwauliza wanafunzi maswali. | *Kutaja aina za hadithi wazijuazo<br>*Kunukuu hoja muhimu<br>*Kusikiliza kwa makini | Je, wanafunzi wameweza kutaja vipera mbalimbali vya hadithi?<br>Je, wanafunzi wameweza kufafanua aina mbalimbali za hadithi<br>Je, wanafunzi wameweza kujibu maswali kuhusiana na hadithi katika kanda za sauti? |
| Ikadiriaji | 15 | *Mwalimu kuwauliza wnaafunzi kusimulia hadithi wazijuazo | *Wanafunzi kusimulia hadithi mmoja mmoja | Je, wanafunzi wameweza kusimulia |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | hadithi zao kwa ufasaha? |
| Hitimisho | 4 | *Mwalimu kuhitimisha somo kwa kuwauliza wanafunzi kutaja na kufafanua vipera vya hadithi | *Wanafunzi kutaja na kufafanua vipera vya hadithi. | Je, wanafunzi wameweza kutaja na kufafanua vipera vya hadithi? |

**Katika maandalizi ya mwalimu pia, mwalimu awapo darasani anatakiwa kuandaa ubao wake kabla hajaanza somo lake. Mgawanyo ubao unatakiwa uwe na mpangilio maalum kama ifuatavyo:**

**Mpangilio wa ubao**

| **Kidato cha I** | **Kiswahili** | **Tarehe 10/2/2013** |
|---|---|---|
| | Fasihi simulizi<br>• Hadithi | |

**Mpangilio wa Ubao**

Hii ni sehemu ambayo hudhihirisha jinsi mwalimu amepanga uabao wake, huku akinukuu muhtasari wa hoja ambazo ni muhimu katika kila somo. Mwalimu anaweza kuugawa ubao wake katika sehemu tatu ambapo sehemu ya kushoto ya ubao huandika masuala ambayo si muhimuna hayatarajiwi kuwa na mpango wowote, yaani sehemu ya mambo ambayo si muhimu. Sehemu ya kati ya ubao ndiyo daftari la mwalimu, na kuandika hoja ambazo ni muhimu na ndiyo hunukuliwa na wanafunzi katika madaftari yao. Sehemu ya kulia ya ubao inaweza kutumika kwa kubandikia chati ikiwa ipo.

**Manufaa ya Ubao**

- Ubao hauhitaji ujuzi au vifaa vingine katika matumizi.
- Anayetumia anaweza kurekebisha au kubadilisha maandishi yake kwa urahisi.
- Ubao una matumizi mengi kulingana na malengo au madhumuni ya somo.
- Hauna gharama kubwa.
- Wanafunzi hupata ujumbe kwa urahisi (ikiwa kazi ina mpangilio mzuri).

**Udhaifu wa Ubao**

- Si nadhifu kwani mwalimu hujichafua kwa chaki na anaweza kukosa mpangilio wa kazi.
- Madhara ya kiafaya yanaweza kumwandama mtumiaji.
- Maandishi hayahifadhiwi kwani yanafutwa punde tu badala ya somo.

**Manufaa ya Andalio la Somo**

- Humhamasisha mwalimu kufanya utafiti kuhusu mada anayoifundisha na kupata maarifa ambayo yanamfanya kuwaongoza wanafunzi ipasavyo.
- Andalio la somo huhakikisha shabaha bunwa ni halisi na zinaweza kukiutekelezeka.

Huwa ni dira ya mwalimu ambayo humwongoza darsani kiasi kwamba hawezi kwenda kando na anayofundisha na kujiepusha na hali ya kuwapotezea wanafunzi wake muda.

Huwezesha usawazishaji wa shughuli za ufundishaji na za ujifunzaji, kiasi ya kwamba vina msambao kabambe katika funzo.

Andalio la somo humhamasisha mwalimu kuandaa zana za ufundishaji, huku zikienda sambamba na mada husika na, hivyo hufanikisha mchakato mzima wa ufundishaji.

Humhamasisha mwalimu kutafakari juu ya mbinu atakazozingatia katika ufundishaji halisi darasani.

Humwezesha mwalimu kupanga muda wake ipasavyo, kwani anajua waziwazi muda atakaotumia katika kila hatua.

Andalio la somo ni kumbukumbu kamili ya kuonesha kuwa mwalimu alifanya kazi na ni thibitisho kamili kwa wale wanaomshuku kuwa hafanyi kazi yake ipasavyo.

Humwezesha mwalimu kuchuja na kubainisha mifano kabambe atakayoitumia katika somo.

Humwezesha mwalimu kupangia kila kikundi cha wanafunzi, kazi yake katika sehemu ya uwasilishaji na kuhakikisha kila mwanafunzi ana la kufanya.

**Kumbukumbu ya yaliyofundishwa**

Kumbukumbu ya yaliyofundishwa ni hadithi ya kazi yote aliyofundishwa na mwalimu katika darasa fulani katika muhula mzima. Kumbukumbu husika inapaswa kudhihirisha kichwa, jina la mwalimyu, shule, kidato na mwaka. Pia, vipengele vingine ambavyo ni muhimu ni pamojana mwezi, juma, kipindi, tarehe, mada, maoni na sahihi ya aliyefundisha. Mada iliyofundishwa ndiyo hunukuliwa, na sio stadi imarishwa. Mwalimu anapaswa kurekodi aliyoyafundisha baada ya kufundisha somo husik. Ikiwa atachelewa kufanya hivyo, ahakikishe amerekodi kazi aliyofundisha kabla ya juma kuhitimika.

**Kielele cha Kumbukumbu ya Yaliyofundishwa**

**Jina la mwalimu:** Kazungu Katana

**Somo:** Kiswahili

**Jina la shule:** Luchelele **Muhula :** 1

**Kidato funzwa:** 1 **Mwaka:** 1

| Mwezi | Juma | Kipindi | Tarehe | Mada/yalifundishwa | Maoni | Sahihi ya mwalimu | Uyakinisho wa mkuu wa shule/idara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1<br>2<br>3 | 10/2/2013<br>11/2/2013<br>13/2/2013 | Fasihi simulizi: Hadithi<br>Kusoma kwa ufahamu<br>Insha: Hadithi ya Kubuni | | | |

**Manufaa ya kumbukumbu ya yaliyofundishwa**

- Ni kipima kazi cha mwalimu kwa kuwa humjulisha aliyoyafundisha katika kipindi fulani.
- Humwezesha mwalimu kukadiria kazi aliyobakiza katika muhula fulani, hivyo ikiwa yu nyuma, anajikaza zaidi kwa kutafuta wakati wa kufidia.
- Humsaidia mwalimu mgeni kufahamu mtangulizi wake alikuwa amekomea wapi katika maazimio ya kazi.
- Humwezesha mwalimu kutorudia mada ambazo alikuwa amefundisha awali, hivyo kutokuwa na uwezekano wa kupotezea wanafunzi muda.

- Safu ya maoni humfaidi mwalimu kwa kumkumbusha jinsi alivyoshughulikia kila mada na kiwangocha uelewa wa wanafunzi. Ikiwa kuna haja ya kurudia mada fulani kama aliyerekodiwa, yeye hufanya hivyo.
- Kupitia hati hii, mwalimu hujua sehemu ambazo atazitathmini wakati wa mtihani.
- Sahihi ya mwalimu ni uthibitisho kamili kuwa yeye ndiye alifundisha, na sio mwengine aliyefanya kazi kwa niaba yake.

**Kumbukumbu ya Tathmini Endelezi**

Kumbukumbu ya tahtmini endelezi ni hifadhi ya takwimu za alama za wanafunzi baada ya kufanya mijarabu na mazoezi katika tathmini endelezi. Alama za kila mwanafunzi hurekodiwa katika daftari maalumu. Mwalimyu anapaswa kutoa mjarabu kwa wanafunzi wake kwa kuzingatiakigezo cha stadi za lugha (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika) kwa sababustadi hizi zinapaswa kuimarishwa kila wiki). Mwalimu anaweza kutahini kila stadi kwa kila wiki. Kifuatacho ni kielelezo kinachoonyesha kumbukumbu ya tathnimi endelezi:

**Kielelezo cha kumbukumbu ya Tathmini Endelezi**

**Jina la Mwalimu:** Kazungu Katana

**Somo:** Kiswahili

**Jina la shule:** Luchelele

**Kidato:** I **Muhula:** I

**Mwaka:** 2013

| **Mwezi** | **Mwezi wa 1** | **Mwezi wa 2** | **Mwezi wa 3** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | 10.1.2013 | 20.2.2013 | 25.3.2013 | | | |
| Stadi | Kusikiliza na Kuongea Upeo/20 | Kusoma kwa ufahamu/sauti/ziada Upeo/20 | Kuandika Insha Upeo/20 | Mtihani wa mwisho wa muhula Upeo% | Wastani Upeo % | Maoni |
| Jina la Mwanafunzi | | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Yaulimwengu Ebrahimu | 10 | | | | | |
| Moyo Kujipenda | 05 | | | | | |
| Karembo Aikande | 06 | | | | | |
| Asha Juma | 02 | | | | | |
| Musa Mamboyote | 01 | | | | | |
| Kapinga Mpingo | 09 | | | | | |
| Tausi Njiwa | 00 | | | | | |
| Mwaka Baraka | 10 | | | | | |
| Mtaula Pendo | 01 | | | | | |
| Karembo Chausiku | 03 | | | | | |

**Manufaa ya Kumbukumbu ya Tathmini Endelezi**

- Honyesha maendeleo ya wanafunzi na humwezesha mwalimu kutoa ushauri ufaao kwa wanafunzi wake.
- Kupitia hati hii, mwalimu anaweza kubainisha wanafunzi walio na shida na kuwashughulikia.
- Hati hi ni ushahidi kamili wa kuwa mwalimu amekuwa akifanya kazi iwapo wakuu wakeau maafisa elimu wanamashaka na utendakazi wake.
- Kumbukumbu ya tathmini endelezi humpatia mzazi na mwalimu nafasi ya jinsi wanavyoweza kusaidiana ili kuboresha matokeo ya mwanafunzi husika.

## Tafakuri ya Somo

## Zoezi la Somo

1. Fafanua uhusiano uliopo baina ya silabasi, maazimio ya kazi na andalio la somo.
2. Andaa somo la kusoma kwa sauti kwa wanafunzi wa kidato cha pili.
3. Kwa maoni yako, mpango wa ubao una manufaa gani katika ufanikishaji wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
4. Eleza umuhimu wa safu ya upimaji katika maazimio ya kazi.
5. Mwalimu ambaye hana hati za taaluma ya ualimu ni sawa na rubani wa ndege ambaye hana dira". Jadili.
6. Eleza jinsi ungefundisha Fasihi Simulizi kwa kidato cha kwanza.
7. Andaa maazimio ya kazi kwa kidato cha nne kwa majuma mawili.

# Somo la Tatu

## Kuchambua Mbinu Mahususi za Kujifunzia na Kuwezeshea Somo la Kiswahili kwa Darasa la Watu Wazima

### Utangulizi

Katika sura hii, tutaangalia mbinu mahususi ambazo zinaweza kutumika kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kwa wanafunzi watu wazima. Mwalimu katika mchakato wa kuwezesha darasa la watu wazima, anatarajiwa kutumia mbinu hizi katika ufundishaji wa masomo mbalimbali yanayoimarisha stadi tofauti tofauti za lugha kama vile kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Katika sura hii maneo yafauayo yatafafanuliwa:

- Eleza maana ya mbinu za kuwezesha.
- Fafanua mbinu za kuwezesha.
- Tumia mbinu mahususi kuwezesha mada za somo la Kiswahili

### Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

▪
▪
▪

### Dhana ya mbinu za kufundishia Lugha

Mbinu za kufundishia lugha ni njia ambazo mwalimu hutumia ili kufanikisha somo lake na kuweza kufikia malengo ambayo mwalimu amejiwekea. Zipo mbinu mbalimbali za kufundishia lugha hususani lugha ya pili. Hivyo basi mwalimu wa lugha anatakiwa kutumia mbinu mbalimbali katika kufundishia lugha. Mbinu nyingi zimaetokana au zinatumika kufundishia lugha ya Kiingereza, hivyo Kiingereza huonekana kama lugha ya kielelezo. Ukirejelea usuli wa mbinu hizo. Kabla ya miaka ya 1970 wataalamu wa lugha walikuwa wakizingatia ufundishaji wa miundo ya sarufi kabla ya kukosolewa. Baada ya kukosolewa ufundishaji wa lugha wakawa wanahimizwa kufundisha lugha

katika muktadha na matumizi yake (David 2010), mpaka kufikia sasa mbinu za kufundishia lugha zimekuwa zikibadilika kwa kubuniwa ili kufikia kiwango cha ufundishaji mzuri na wenye ufanisi yaani matokeo mazuri.

Hata hivyo hakuna mbinu tunayoweza kusema inafaa zaidi kuliko nyingine, kwani kila mbinu ina ubora na udhaifu wake inategemea mwalimu anaitumia vipi hiyo mbinu husika. Mbinu za kufundishia lugha ya pili au ya kigeni zipo nyingi kutokana na mitazamo tofauti ya mabadiliko katika ufundishaji wa lugha.

Katika kufundisha na kuwezesha lugha, ilikuwepo mikabala na mbinu mbalimbali. Lakini mbinu iliyoonekana kuwa na mashiko na yenye ufanisi ni mbinu ya kimawasiliano ambapo mbinu nyingi za kufundishia lugha kwa sasa zimechota sifa za mbinu hiyo ambayo inajikita kwenye mawasiliano Zaidi. Kabla hatuajaingia kwenye mbinu mahususi za kuwezeshea na kujifunzia Kiswahili, hebu tuone sifa za mbinu hii mama ambayo inatumika kufundishia lugha.

## Mbinu za Kufundishia Lugha ya Kiswahili kwa darasa la watu wazima

Zifuatazo ni mbinu mahususi za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa darasa la watu wazima:

- Mbinu au mkabala wa Kimawasiliano
- Kutumia mbinu za majadiliano katika vikundi
- Kutumia mbinu ya kuuliza na kujibu maswali
- Kutumia Mbinu ya Mhadhara
- Kutumia Mbinu ya Maagizo (igizo dhima, mgando na igizo bubu)
- Kutumia Mbinu ya matuimizi ya wageni waalikwa
- Kutumia Mbinu ya kazi mradi
- Kutumia Mbinu ya maelezo
- Kutumia Mbinu ya hadithi
- Onyesho mbinu
- Mbinu ya Matembezi ya galari

- Mbinu ya Changanya Kete
- Mbinu za ziara za kielimu
- Mbinu ya Utambuzi

Ndugu mwanafunzi, kabla hatuaanza kuchambua na kufafanua mbinu mahususi za kufundishia somo la Kiswahili hebu tupitue mkabala wa uwezeshaji lugha ambao unapendekezawa na wataalam wengi utumike katika kufundishia na kuwezeshea somo la kugha. Mkabala huo unajulikana kama Mkabala wa Kimawasiliano (Communicative Approach) ambao unaelekeza misingi na kanuni za ufundishaji way lugha kama ifuatavyo:

## Asili ya Mkabala wa Kimawasiliano

Katika miaka ya 1960 na1970 uwezeshaji wa somo la lugha ulianza kuboreshwa na mabadiliko makubwa ya mitaala na mbinu za kuwezeshea yalianza kufanywa. Hatua hii ilichochechewa na kuwapo na mbinu za uwezeshaji lugha zinazowaongoza wanafunzi kukariri na kurudiarudia miundo isiyo na maana yoyote.

Mitaala ilitakiwa kujadili mahitaji ya wanafunzi tofautitofauti. Kimsingi mbinu hii mkusanyiko wa mawazo mbalimbali kutoka katika vyanzo mbalimbali kutoka katika vyanzo yanakubalika kama mbinu bora za kuwezeshea somo la lugha.

- Mbinu hii ilishika mizizi na kupanuka zaidi nchini Uingereza katika miaka ya sabini. Lengo azma ya kuzuka kwa mbinu hii ilikuwa ni kukidhi na kufanikisha mawasiliano na sio kukuza umilisi wa miundo ya sarufi au viambajengo vya lugha husika.
- Mbinu hii iliibuka wakati wa vita vya b pili vya dunia wakati ambao askariwaliotakiwa wajue lugha za mataifa mbalimbali.
- Mbinu hii imechukua misingi yake kenye nadharia ya utabia kwa kiasi kikubwa.
- Kwa hiyo lengo lake kubwa lilikuwa kukidhi matakwa ya wanaojifunza lugha ya pili katika mawasiliano.
- Mbinu hii inapotumiwa kufundisha lugha ya Kiswahili itafundishwa katika uamilifuwake, ikiwa na maana kwamba kufundisha iliiwawezeshewanaokitumia kuwasiliana na sio umulisi wa kaida/kanuni zake.

- Waasisi wa mbinu hii walishikiia kwamba /kuwa jukumu kuu la lugha ni kufanikisha maingiliano na mawasiliano katika jamii. Wao walihimiza kuwa mawasiliano yatendeke katika muktadha wa mazungumzo na majadiliano.
- Mwalimu anaye tumia mbinu hii anaweza kuwagawa wanafunzi katika vikundi vidogovidogo ili waweze kufanya mazoezi ya kutosha na kujenga umahiri wa kuwasiliana ipasavyo ubora wa mbinu hii.
- Kulingana na waasisi wa mbinu hii mwalimu ana nafasi kubwa ya kuwahimiza wanafunzi wake kuzungumza kwa ufasaha, kuwapatia fursa ya kuweza kujadiliana na kuzungumza kwa lugha wanayofundishwa.
- Ni mbinu yenye misingi nyumbufu.

**Misingi mikubwa ya mbinu hii ni kama ifuatavyo:**

1. Lugha ni chombo cha mawasiliano hivyo ufundishaji uzingatie ujengaji wa umahiri wa kimasiliano.
2. Mitaala ni sharti izingatie ujenzi wa uwezo wa wanafunzi katika kuwasiliana
3. Lugha isifundishwe kidhahania ni sharti mwezeshaji atengeneze muktadha ambamo lugha hiyo itatumika
4. Muktadha huo ujengwe kijografia kwa kutumia zana na vifaa vingeine muhimu
5. Wanafunzi wapewe fursa ya kufanya matendo mbalimbali darasani nanje ya darasa yatakayo wafanya watumie miundo ya lugha iliyokusudiwa.
6. Msisitizo uwe katika kueleweka kwa ujumbe wanaouwasilisha au kazi/vitendo wanavyofanya kuliko usahihi wa miundo wanayoijengakama inavyotokea mtoto ajifunzapo lugha ya kwanza kwa mawazo ya Chomsky.
7. Uwezeshaji kwa kutumia mbinu hii unamjali mwanafunzi zaidi.
8. Madarasa yatoe fursa ya kutosha ya kutumia lugha katika mazingira halisi na hivyo kutoa kutoa fursa ya kufanya mawasiliano halisi.

9. Utumizi wa jozi na majadiliano katika vikundi ni jambo la msingi sana.
10. Msisitizo uwekwe kwenye ujenzi wa stadi za kuzungumza na kusikiliza
11. Wanafunzi wapewe fursa ya kufanya makosa na wajifunze kutokana na makosa wafanyayo.
12. Kufanya makosa ni sehemu ya kujifunza lugha kwamba kuwarekebisharekebisha wajifunzao wajifunzao hakujengi msingi imara wa kujifunza lugha.
13. Pamoja na msisitizo kuwekwa katika ujenzi wa stadi za kusikiliza na kuzungumza, stadi za kuandika na kusoma pia huzingatiwa.
14. Miundo inaweza kuendelea kufundishwa lakini siyo kwa msisitizo mkubwa hususani upande wa kanuni zake.
15. Vifaa vya kufundishia ni shari viendane na maisha ya wanafunzi na view halisi.
16. Zana za kuona/maono ni muhimu zitumike katika uwezeshaji kwa kuwa zinavuta nadharia na kuhamasisha
17. Utumiaji/ujifunzaji lugha nisharti uzingatie miktadha ya kijamii na kiutamaduni.
18. Mwezeshaji anatakiwa kuwaongoza wanafunzi wajifunze ila asiwabane sana awape uhuru kwani kuwasahihisha wanafunzi wakati wanawasiliana wao kwa wao kunaharibu mtiririko wa mawasiliano na kudhohofisha jitihada za kulifikia lengo la kimawasiliano hivyo marekibisho kama ni ya lazima yafanywe mwishoni.

Mwalimu anatarajiwa kutumia mbinu hizi katika ufundishaji wa masomo mbalimbali yanayoimarisha stadi tofauti tofauti za lugha. Baadhi ya mbinu hizi ni pamoja na;

## Maelezo

Maelezo ni ufafanuzi wa kitu Fulani. Mtu anapotoa maelezo huwa anapambana kwa kina kuhsu kitu au jambo Fulani Maelezo ni moja wapo ya mbinu mwalimu anaweza kuitumia kuelezea jambo jipya. Maelezo ni mbinu mwafaka inayoweza kutumiwa kufafanua mafumbo, msamiati mpya, maneno yenye maana zaidi ya moja

(vitawe) au maneno yenye maana sawa (visawe). Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu hii pamoja na mbinu ya kuuliza na kujibu maswali ambapo mbinu ya pili itashadidia umakinifu wa wanafunzi. Ikiwa mwalimu atazingatia mbinu ya maelezo peke yake, wanafunzi hawatamanikika zaidi ikilinganishwa na anapoitumia pamoja na mbinu ya kuuliza na kujibu mawali.

**Uzito wa Mbinu ya Maelezo**

- Ufafanuzi wa baadhi ya hoja unawafikia wanafunzi kwa njia nzuri zaidi.
- Maelezo huwa ni ya kina na humfanya mwanafunzi kuelewa mambo kwa undani zaidi.
- Mbinu hii hufana kwa kiwango Fulani katika maelezo ya msamiati mpya.

**Udhaifu wa Mbinu ya Maelezo**

- Ili mbinu ifaulu ipasavyo haiwezi kusimama peke yake na uhitaji msaada wa mbinu ya kuuliza na kujibu maswali.
- Ikiwa mwalimu ana matatizo ya kuzungumza Kiswahili fasaha, wanafunzi hawatamwelewa vizuri.
- Ikiwa mwalimu alikuwa anafundisha msamiati mpya, mbinu ya maelezo inaweza kuchangia wanafunzi kuibuka na kamuzi ndogo ambayo haiwasaidii kuelewa maana kimuktadha. Hivyo basi, mbinu hii inahitajika kutumiwa kwa tahadhari sana katika vidato vya kwanza na vya pili.

## Kuuliza na Kujibu Maswali

Mbinu ya uulizaji na ujibuji wa maswali inaweza kutumika kawa vidato vyote, kuanzia kidato cha kawanza hadi cha sita. Maswali ambayo anawauliza wanafunzi wake lazima yaendane na kiwango cha wanafunzi. Wanafunzi wa kidato cha kawanza cha tatu na cha nne, maswali yanapaswa kuwa mazito kidogo, (hata hivyo yasiwe mazito kiasi cha kutinga ufahamu wa wanafunzi).

Mwalimu anapouliza maswali lazima asigatie kiwango cha wanafunzi na uelewa wao. Hivyo basi, maswali wanayotarajia ni

maswali ambayo ni yenye kiwango cha ufafanuzi, ufahamu, maswali tumikizi, uchanganuzi, usanisi na tathmini. Mwalimu anatahadharishwa kuwa, anapouliza wanafunzi maswali anahitaji kuzingatia mambo yafuatayo:

- Somo awali tajiriba na kiwango cha mwanafunzi
- Mwalimu aulize swali na kutaja kwa jina mwanafunzi atakayelijibu, lakini sio kuanza kwa kumtaja amwanafunzi na baadaye kuuliza swali. Hali hii inapotokea, wanafunzi wale wengine watachukulia kuwa swali lilikuwa la mwanafunzi aliyetajawa na mwalimu tu.
- Maswali yawe ni ya moja kwa moja kiasi cha kutozua utata wowote.
- Mwalimu anatahadharishwa kutouliza maswali yanayowashawishi wanafunzi kujibu kwa halaiki.
- Mwalimu atumie msamiati unaoeleweka kawa wanafunzi. Mwalimu anatahadharishwa kutojitapa anapowauliza wanafunzi maswali, kwani ya hali mwalimu kujifanya anajua sana na kuwa na maringo maringo mbele ya wanafunzi itawafanya waanze kumchukia na hata kulichukia somo lenyewe.
- Mwalimu anapowauliza swali awapatie wanafunzi muda wa kufikiria na wanaposhindwa ibadilishe namna ya kuuliza swali hilo upya.
- Mwalimu anatahadharishwa kutojibu swali ambalo limemshinda mwanafunzi lengwa, lakini alielekeze kwa mwingine ajaribu kulijibu.
- Mwanafunzi anapojibu swali kwa usahihi, mwalimu anahimizwa kumpongeza na anapokosea asimkaripie, bali amhimize kwa maneno ‘ulikuwa karibu kupata jaribu tena, umekosea kidogo sana, jaribu tena’. n.k.

**Umuhimu wa Mbinu ya Kuuliza na Kujibu Maswali**

- Hubeba fikira za wanafunzi.
- Maswali. Mwalimu anafahamu iwapo anaendelea vizuri katika somo. Pia mbinu hii inasaidia kukadiria uelewa wa wanafunzi katika hatua moja, kabla ya kuuza hatua mpya.

- Humsaidia mwalimu kufahamu iwapo wanaenda pamoja na wanafunzi wake katika kipindi husika.
- Mbinu ya maswali humsisimua na kuchangamsha mwanafunzi, huku maswali yakimweka katika hali ya tamakani.
- Mbinu hii huchangia kukamilisha mbinu ya maelezo.

**Udhaifu wa Mbinu ya kuuliza na kujibu Maswali**

- Haitilii maanani wanafunzi ambao wana matatizo ya kuona au kusikiliza.
- Wakati mwingine, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi ambao wanaonyesha ari ya kujibu maswali kwa kunyanyua mikono na kuwa puuza wale wengine.
- Baadhi ya walimu huwa hawana subira wakati wameuliza maswali, kwani hutarajia jibu, papo kwa hapo, bila kuwapatia wanafunzi muda wa kufikiria na kuitikia ipasavyo.
- Kuna uwezekano wa kubuni maswali ambayo yanadhihirisha utata na kuwakanganya wanafunzi.
- Mara nyingi wanafunzi wenye haya hawapati nafasi ya kuulizwa maswali. Halikadhalika baadhi walimu hawawashajiishi wala kuwahamasisha kuuliza maswali, katikati ya kipindi na hata baada ya kipindi.
- Mbinu hii haiwezi kujitokeza bila msaada wa mbinu zingine.

## Mbinu ya Mjadiliano

Majadiliano ni mazungumzo baina ya watu kuhusu jambo Fulani. Kimsingi mbinu ya majadiliano huchangia kuimarisha stadi ya kusikiliza na kuongea, huku wanafunzi wakiboresha matamshi yao. Mbinu ya majadiliano hutoa mchango mkubwa kwa somo la fasihi na hasa katika uchambuzi wa vipengele mbalimbali katika kazi za fasihi. Kupiti, majadiliano, mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi wake kuchambua dhamira, ujumbe falsafa na msimamo wa mtunzi katika fasihi.

Pia mbinu hii, hurahisisha kazi ya mwalimu katika uchambuzi wa fani katika fasihi. Ili kufaulisha mbinu hii, mwalimu hujitokeza kamasihi. Ili kufaulisha mbinu hii, mwalimu hujitokeza kama

kinara asiye na maamuzi yoyote katika kajadiliano. Jukumu kubwa la mwalimu ni kuwapatia wanafunzi wake mwelekeo katika mjadala kwa kuwaongoza ili wasiende nje ya malengo mahsusi ya somo.

Majadiliano yanaweza kuandaliwa kwa kuzingatia njia tatu: mazungumzo ya ghafla, mazungumzo ya hadhara na mjadala au midahalo. Katika mazungumzo ya ghafla, mwalimu huandika vijikaratasi vyenye mada jadiliwa na kuwapa wanafunzi wajadiliane, papo kwa hapo, bila taarifa ya awali. Mazungumzo haya hayachukui muda mrefu. Pia mazungumzo ya hadhara ni aina ya mazungumzo ambayo mwalimu huandika mada mbalimbali na kuwapa wanafunzi ili wajitayarishe kwa mjadala kwa kipindi ambacho kitafuata. Hivyo basi, tofauti na mazungumzo ya ghafla mwalimu huwapatia wanafunzi muda wa kujipanga na kujiandaa. Mdahalo huhusisha wanaopinga na wanaounga mada fulani mkono. Mwalimu huwataarifu wanafunzi na kujipanga mapema katika vikundi viwili (wanaounga mkono na wanaopinga). Mdahalo huu huwa na kinara na katibu anayenukuu hoja za kila mjumbe. Hatimaye, badala ya mdahalo katibu hutangaza mshindi kwa idhini ya mwalimu.

**Uzito wa Mbinu ya Mjajadiliano**

- Huchangia kukuza stadi za kusikiliza na kuongea
- Hukuza ujasiri miongoni mwa wanafunzi
- Hukuza matamshi bora miongoni mwa wanafunzi
- Huwa ni kigezo au mizani ya kupima wanafunzi katika stadi za kusikiliz na kuongea.
- Huchangia kukuza lugha na sarufi ya wanafunzi kwa jumla
- Huwawezesha wanafunzi kupanua msamiati wao wanapojadiliana.
- Wanafunzi hupanua fikra zao kuhusu masiala wanayojadiliana
- Majadiliano huwasaidia wanafunzi kujifunza na kuzoea kufikiria kwa kasi huku wakipanga mawazo yao katika mantiki inayokubalika.

**Udhaifu wa Mbinu ya Majadiliano**

- Wanafunzi wenye ujasiri huishia kutawala majadiliano
- Mdahalo huhitaji muda mrefu kwa ajili ya maandalizi ya awali
- Mchemko wa hasira unaweza kujidhihirisha miongoni mwa wanafunzi, hali ambayo huathiri mahusiano darasani.
- Muda unaweza kupotezwa ikiwa wanaojadiliana wataishia katika kupotoka kihoja na kuzungumzia masuala yasiyoelngwa katika mjadala.
- Kuna uwezekano wa mwalimu kukosa kudhibiti darasa, hali ambayo kuchangia kuharibu muda wa wanafunzi.
- Huenda wanafunzi wenye ukwasi w alugha ndiyo watakaojitolea kujadiliana, huku wenye haya wakichelea kujitokeza. Hivyo basi, hali inapodhihirika, mwalimu anapaswa kuingilia kati kwa kuwateua yeye wanafunzi mwenyewe.

## Mbinu ya Mhadhara

Mbinu ya mhadhara ni aina ya ufundishaji ambao huhusisha mwalimu tu bila kuwashirikisha wanafunzi. Mbinu hii humfanaya mwanafuzni kuwa mpokezi na msikilizaji badala ya mwalimu kumhusisha katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Njia hii ni nzuri wakati wa kufundisha somo la fasihi. Mwalimu huzungumza kwa muda mrefu, huku wanafunzi wake wakimsikiliza tu. Hata hivyo, kwa njia moja au nyingine anahitaji kuwashirikisha wanafunzi.

## Mbinu ya Maigizo

Ni kitendo cha kuigwa. Mwalimu anapaswa kuwa kielelzo cha mchakato mzima wa uigizaji. Wakati wa kutumia mbinu hii mwalimu anapaswa kushiriki katika uigizaji wa jukwaani. Kupitia uigaji, mwalimu anaweza kuigiza vitenzi mbalimbali, hususani, kutembea, kukumbia na kusimama, kutambaa, kucheza, kuandika. Pia mwalimu anaweza kufundisha vielezi vya jinsi kwa kutumia mbinu ya uigizaji. Mara nyingi mbinu hii inahitaji ufafanuzi wa moja kwa moja. Mbinu hii ni nzuri katika ufundishaji wa sarufi, fasihi simulizi na utanzu wa tamthilia.

## Matumizi ya Hadithi

Japo hadithi inaweza kuchukua nafasi ya somo linaloimarisha stadi za kusikiliza na kuongea, wakati huo huo, hadithi inaweza kutumika kama mbinu ya kufundishia. Hadithi inaweza kuwafanya wanafunzi kuwa katika hali ya tamakani. Iwapo mwalimu atagundua wanafunzi wake wanasinzia darasani, anaweza kuwasimulia hadithi. Hadithi lazima iwe na uhusiano na mada husika, hivyo mwalimu anahitaji kuwa mbunifu zaidi. Mwalimu anapotonga hadithi, anatahadharishwa kutoikamilisha ili iwaweke wanafunzi katika hali ya taharuki ambapo hali hii itawafanya wanafunzi kuwa kayika hali ya tamakani na kumsikiliza mwalimu huku wakiwa na matarajio ya mwalimu ya kuhitimisha hadithi yake.

## Matumizi ya Wageni Waalikwa

Wageni waalikwa ni wataalamu katika tasnia fulani. Lengo kuu la kuwaalikwa wageni waalikwa ni kufaulisha somo fulani kwa sababu ya ujuzi walio nao kuhusu somo husika. Wageni hawa huwa ni watu wenye maarifa katika uwanja fulani, kwa mfano mgeni mwalikwa anaweza kuwa na tajiriba pana katika ufundishaji hivyo kuonyesha umahiri katika uwasilishaji wake.

## Mbinu ya Vikundi vya Majadiliano

Mbinu hii huhusisha vikundi mbalimbali vya wanafunzi ambavyo huungana ili kujadiliana kuhusu masomo mbalimbali. Vikundi hivi huundwa na mwalimu huku akitilia maanani hulka na uwezo wa wanafunzi. Mwalimu anatakiwa kuchanganya wanafunzi werevu na wanafunzi ambao ni wa hali ya chini. Vikundi hivi ni muhimu mwalimu anapovitumia kujadiliana kwa kutoa mchango kuhusu mada iliyofundishwa. Mwalimu anaweza kuwaganya wanafunzi wake katika makundi ya watu watano au sita. Wakati mbinu hii inatumika, mwalimu anashauriwa kuwaongoza wanafunzi wanapojadiliana ili kusitokee wengine wanaozembea darasani.

## Mbinu za Kazi Mradi

Mbinu ya kazi mradi humshirikisha mwanafunzi kwa njia ya moja kwa moja. Mwanafunzi hupew kazi Fulani na mwalimu na baadaye hutarajiwa kuiwasilisha kwa mwalimu au darasani. Kazi mradi huwa na chembechembe za utafiti na umuhitaji mwanafunzi kuingia maktabani na uwandani na kufanya utafiti. Mbinu ya

kazimradi humfanya mwanafunzi kusoma na kuyapanga mawazo anayoyasoma au kuyaoanisha na hatimaye kuyaandika. Mbinu hii inamhitaji mwanafunzi binafsi kukusanya data, kuichanganua na kuhifadhi kimaandishi na kuwasilisha matokeo ya kazi mradi.

## Mbinu ya Utumiaji wa Kanda na Santuri

Kanda au santuri ni vifaa vya kieletroniki ambazo hutumika katika uwasilishaji wa somo. Mwalimu anaweza kuandaa somo na kulipeperusha hewani kwa mitambo ya elektroniki kwa wanafunzi wake. Kanda na santuri huchukua nafasi ya mwalimu wa kawaida. Mwalimu anahitajika kuhakikisha rungoya au runinga inayopeperusha somo husika iko katika somo husika iko katika hali nzuri. Mbinu hii ni muhimu kwani huchangia katika kuimarisha stadi za kusikiliza na kuongea miongoni mwa wanafunzi, husiadia kuchochea fikra za wanafunzi ili waweze kujieleza.

## Mbinu ya Kinuruweo

Kinuruweo ni istilahi inayosimamia tafsiri ya maneno power point ya Kiingereza. Istilahi hii imeundwa kutokana na maneno mawili yaani nuru + kiweo. Mbinu hii hutumiwa pamoja na tarakilishi mpakato katika kufundishia masomo kama Fasihi Simulizi na matamshi bora. Mwalimu huandaa nukuu, michoro, majedwali pamoja na picha kwa kutumia tarakilishi mpakato. Kinuruweo humsaidia kurusha yote aliyoayaandaa kwa ajili ya wanafunzi kuandika au kusoma ili waweze kushirikishi katika somo husika.

## Mbinu ya Ziara ya Kielimu

Mbinu hii hutumiwa na mwalimu punde anapowatoa wanafunzi wake nje ya darasa na kuzuru mahali au maeneo mengine ili kujifunza jambo fulani. Mwalimu anatahadharishwa mahala ambapo atazuru pamoja na wanafunzi wake kuwa lazima pahusiane na mada anayotaka kufundisha. Ikiwa anataka kufundisha somo la msamiati wa sokoni au mahakamani atahitajika kupanaga safari ya kuzuru soko au mahakamani. Kabla ya ziara ya kielimu kufanyika kuna mipango ya awali inayohitajika kutimizwa kama ifuatavyo:

-Kuomba idhini ya kutembelea sehemu husika

-Kumwelewesha mwalimu kushirikiana na walimu wengine wa somo.

-Kuwaandaa wanafunzi wake kwa kuwaelekeza kuhusu maswali watakayouliza

-Kupanaga masuala ya usafiri na chakula cha wanafunzi

-Kuandika ripoti ya kile walichojifunza

## Changanya Kete

Ni mbinu shirikishi ambayo mwezeshaji huandaa maswali katika vikundi halafu mwanafunzi mmoja kutoka katika kila kikundi huenda katika kundi lingine na kushiriki katika kundi hilo na kuunda makundi mengine. Baadaye wale wanafunzi waliohamia kwenye makundi hayo hurudi kwenye makundi ya awali. Kimsingi mbinu hii huchanganya wanafunzi kutoka makundi tofauti tofauti. Kwa kuhitimisha, tunaweza kusema kuwa mbinu za kufundishia somo la Kiswahili zinaweza kugawanywa katika makundi mawili yaani mahususi na mbinu saidizi. Mbinu mahususi ni zile tulizojifunza katika sura iliyopta ambazo ni za kimapokea zaidi. Mbinu saidizi hujulikana kama mbinu za kisasa ambazo ndiyo zinatumika sana katika.

## Mbinu ya Uigizaji Kivitendo

- Ni mbinu ambayo inahusissha uzingatiaji wa vitendo katika kufundisha lugha ya pili iliyoasisiwa kule marekani miaka ya 1920. Mbinu hii huzingatia matumzi ya vitendo katika ufundishaji.
- Ili kufanikisha mbinu hii mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa wanafuzni wake wana umilisi wa usiklizaji, kwani usikilizaji ukiimarika, nao uzungumzaji huimarika.
- Inaamika kuwa mwanafunzi ambaye ana uwezo wa kusikiliza na kuongea atakuwa katika nafasi bora ya kuigiza vitendo na kuitika maelekezo /amri mbalimbali zinazotolewa na mwalimu bila matatizo yoyote hali ambayo husarahisisha ufundishaji wa lugha nya pili.
- Katika uigizaji wa vitendo wanafunzi hushirikishwa katika katika urusdaiji na ukaririshwaji wa vitendo darasani.
- Ili wanafunzi wajihisi kuwa wapo katika mazingira ya yanafaa ya ujifunzaji wa lugha ya pili, wanahitajika kushirikiwsha katika miktadha mbalimbali ambamo lugha husika hutumika. Kwa mfano katika kufundisha mada ya mitindo mbalimbali ya lugha, wanafuzni wanaweza kutembelea, kufanya ziara katika maeneo ambamo lugha hizo hutimika, kwa mfano, kuembelea shambani, dukani kanisani, mahakamani, kijiweni, bandarini,

hospitalini, sokoni, kituo cha daladala, garimoshi n.k. Hii itamsaidia mwanafunzi kupata uhalisia wa mtindo husika wa lugha kulinagana na mukatadha wa amtumizi.

- Aidha, ili kufanikisha ufundishaji wa lugha ya pili, mwalimu anaweza kutumia amri mbalimbali, kufundishia mada kama vitenzi kwa kuwaita wanafuzni kuafanya matendo kama, funga mlango, simama, kaa, kimbia, chutama n.k. Pia kupitia mbinu ya uigizaji kivitendo mwalimu wa Kiswahili anaweza kufundisha mada ya vielezi vya jinsi, mithili ya, tembea kiaskari, fanaya kazi ovyo ovyo, cheke kiungwana n.k.

## Mbinu nyinginezo za kufundishia na kujifunzia Lugha

Mbali na mbinu zilizotajwa hapo juu pia kuna mbinu zingine zinazoweza kutumika kufundishia lugha.

**Mbinu ya Utambuzi (Cognitive Code Method)**

1. Watetezi wa mbinu hii ni wanaisimu zalishi na wanasaikolojia tambuzi.

2. Mbinu hii inachota sifa za misingi ya Nadharia ya Utambuzi ya Jean Piaget. Nadharia hii illibuka miaka 1920 kabla ya mwitikio wa uhakiki wa nadharia zilizotangulia.

3. Mbinu hii pia ilirekebisha mbinu ya tafsiri sarufi na mbinu ya moja kwa moja yaani kufundisha bila kutafsiri.

4. Nadharia hii inasisitiza kumpa mwanafunzi uwezo wa kuelewa mfumo wa lugha ya kigeni, kisha aendelee yeye mwenyewe kujifunza baada ya kuelewa mfumo huo.

5. Mbinu hii inatambua kuwa mwanafuzni huyu ana akili ya kuweza kujifunza kuhusiana na lugha ile yeye mwenyewe (mtu huzaliwa na uwezo wa kujifunza kutokana na kifaa kilichopo kwenye ubongo KIULU yaani kifaa cha kuamilimi lugha. (LAD).

Kwa mantiki hiyo mbinu hii inashadadia mawazo ya Chomsky (1957 na 1968) kwamba umilisi alionao mwenyeji wa lugha ni kama mtambo unaomwezesha kuzalisha maelfu ya tungo mbambali katika lugha yake yaani Umilisi na utendaji (Competence na Performance).

6. Mkabala au mbinu hii inapinga mkabala wa utabia kwamba kujifunza lugha kunatokana na utambuzi na sio tabia ya kurudiarudia yaani uigaji.

7. Kwa kuhitimisha, mbinu hii inazingatia zaidi kumpa mwanafunzi kanuni za msingi za lugha kigeni (lugha anayojifunza na mazoezi yanayoshadadia maana).

**Mbinu ya Moja kwa Moja**

- Nadharia hii ilianzishwa na mtaalam aitwaye Gouin (1880). Mbinu hii huzingatia zaidi stadi ya mazungumzo ambayo hupangiliwa kwa makini, hatua kwa hatua. Mbinu hii ilizaliwa kutokana na mbinu ya Tafsiri Sarufi ambayo iliibuka mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 na kuchukua nafasi ya mbinu tangulizi ya Tafsiri Sarufi.
- Kimsingi mbinu hii ilisisitiza ufundishaji wa lugha ya pili kwa kutumia lugha hiyohiyo jambo ambalo liliwakatisha walimu tamaa kwa kutotumia tafsiri yoyote ile katika ufundishaji wao. Wafuasi wa mbinu hii waliamini kuwa wanaojifuzna lugha ya pili wanaweza kujifunza kama wanavyojifunza lugha ya kwanza pasipo kuzingatia lugha nyingine katika ujifunzaji.
- Kutokana na mtazamo huo, waitifaki waliamini kuwa anayejifunza lugha ya pili ni sawa na mtu anayejifunza lugha ya kwanza moja kwa moja bila kujiegemeza katika tafsiri yoyote, Hivyo wanachukulia kwamba anayejifunza lugha angejifunza kama mtoto anayejifunza lugha ya mama kwa kukumbana nayo moja kwa moja.
- Kutokana na msimamo au mtazamo huu kuna ukweli Fulani. Katika hali halisi hakuna mtu anayemfasiria mtoto kaida za lugha anayojifunza mtoto.

**Ubora wa Mbinu Hii**

(i)Husaidia zaidi stadi ya mazungumzo

(ii)Humsaidia kukuza msamiati

(iii)Mbinu hii inaongeza umilisi na utendaji

(iv)Huzingatia zaidi stadi ya mazungumzo iliyopangiliwa hatua kwa hatua.

(v)Huzingatia msamiati wa lugha husika ambao hutawala msamiati wa mafunzo.

**Udhaifu wa Mbinu Hii**

(i)Stadi ya kuandika haipewi uzito unaostahili

(ii) Haizingatii uchanganuzi wa miundo ya kisarufi

**Jinsi ya Kutumia Mbinu Hii**

1. Kwa kutumia mbinu hii somo huweza kuanza na hadithi fupi, michepuo, majadiliano katika lugha lengwa kwa ajili ya mawasiliano.
2. Pia mawasiliano yanatolewa kwa mazungumzo, picha na vielelezo.
3. Lugha ya awali yaani lugha ya mama haitumiki kabisa au kavu.
4. Mazoezi ni maswali katika lugha lengwa.
5. Sarufi hufundishwa kwa kuzingatia muktadha wa vielelezo
6. Vitenzi sahihi hutumika mwanzo na baadaye hunyambuliwa
7. Wanafunzi wa kiwango cha juu husoma fasihi kwa ajili ya ufahamu.
8. Ufafanuzi wa kisarufi hautumiki.
9. Utamaduni unaohusishwa na lugha lengwa unatumika kimatumizi.

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa wakati wa kutumia mbinu hii walimu wanahimizwa kuzingatia matumizi ya uigizaji na vifaa kama vielelezo ili mwanafunzi aweze kutambua kanuni za kisarufi mwenyewe katika lugha husika kupitia vielelezo vinavyotumika.

**Mbinu ya Usomaji**

Hii ni mbinu nyingine ambayo inatumika katika kufundishia. Hii pia huitwa mbinu ambatano ambayo hutumika kufundishia na kujifunzia. Mbinu hii hutumika kwa wale wanaojifunza lugha kwa

malengo ya kuendeleza uwezo wao wa kusoma na kumaizi historia ya kugha husika ambayo wanajifunza.

**Sifa ya Mbinu ya Usomaji**

1. Sarufi inayohusika katika usomaji ndiyo inayohusika.
2. Utamkaji hautiliwi mkazo bali usomaji peke yake hutiliwa mkazo.
3. Ufundishaji wa msamiati huratibiwa hivyo kufanya msamiati kukuzwa kwa haraka.
4. Msamiati ni muhimu kuliko sarufi.
5. Tafsiri haitiliwi mkazo

## Mbinu Pendekezi (Mbinu ya Sajestopedia) (Suggestopidia)

Sajestopidia ni neno lililoundwa kutokana na maneno mawili ya lugh ya Kiingereza yaani ***suggestive*** na ***pedalogy***. Kwa hiyo neno sajestopidia limetoholewa kutoka katika neno la lugha ya Kiingereza lijulikanalo kama suggestopedia kama Mbinu hii imeasisiwa na Georgi Lozanov.Mwasisi huyu anaamini mbinu hii ina uwezo mara tatu zaidi ya mbinu nyingine za kufundishia lugha iwapo itatumika vizuri. Msingi mkubwa wa mbinu hii ni mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ambapo anayejifunza lugha anatakiwa kutumia milango yote ya fahamu kwa ufanisi katika kuwezesha somo la lugha. Hivyo basi, ili mbinu hii iweze kutumika kwa ufanisi ni vema mazingira ya kujifunza yawe na ukwasi wa vifaa vya muziki, matumizi ya nyimbo na maigizo.

Ufundishaji kwa kutumia mbinu hii unahusisha hatua 4 muhimu ambayo ni kama ifuatavyo:

**1. Utangulizi wa mada husika**

Mwalimu anashauriwa kuwafanya wanafunzi wawe katika ari ya kujifunza. Wavute utayari utakaowawezesha kujifunza kwa urahisi na kwa furaha.

**2. Uwasilishaji wa mada**

Mwalimu katika hatua hii anashauriwa kuwasilisha vifaa/zana zitakazotumika kujifunzia. Matendo ya ujifunzaji yaende sambamba na muziki laini ili kuwaburudisha wanafunzi.

**3. Udurusu wa kilichofundishwa**

Hatua hii inahitaji wanafunzi wawe watulivu (relax) na kusikiliza mziki laini huku wakidurusu walichojifunza taratibu.

**4. Vitendo**

Katika hatua hii mwalimu anapaswa kuwaongoza wanafunzi kufanya vitendo kuhusiana na walichojifunza, vitendo hivyo vihusishe michezo, mazoezi ya lugha kwa vitendo nk.

Kwa kiasi kikubwa mbinu hii ni ile inamshughulisha mwalimu zaidi kuliko mwanafunzi hususani pale anapofanya maandalizi. Kwa upande wa walimu, Lozanov anashauri na kupendekeza vitu vifuatavyo:

1. Walimu wawe na uwezo wa kufundisha mambo mengi kwa pamoja/wakati mmoja.

2. Walimu wafundishe kwa kuwianisha kati ya yale yahusuyo ulimwengu halisi kwa wakati huu naujao na yale yenye faida baadaye.

3. Nivema walimu wajiamini na wajidai kwa weledi wao.

4. Ni lazima awapende wanafunzi wake na ashiriki katika vitendo vya kujifunza pamoja na wanafunzi.

Nadharia hii inasisitiza kwamba mazingira na hali ya kujifunzia darasani ni muhimu sana ili kumfanya mwanafunzi afikiri vizuri na mwenye kujiamini.

Lozanov alikuja na mbinu hii baada ya kuona kuwa mbinu za awali zilikuwa na mtazamo hasi kwani hazikumuweka huru mwanafunzikutokana na magumu/vikwazo katika mchakato wa kujifunza.

## Mbinu ya Utambuzi (Cognitive Code Method)

1. Watetezi wa mbinu hii ni wanaisimu zalishi na wanasaikolojia tambuzi.

2. Mbinu hii inachota sifa za misingi ya Nadharia ya Utambuzi ya Jean Piaget. Nadharia hii illibuka miaka 1920 kabla ya mwitikio wa uhakiki wa nadharia zilizotangulia.

3. Mbinu hii pia ilirekebisha mbinu ya tafsiri sarufi na mbinu ya moja kwa moja yaani kufundisha bila kutafsiri.

4. Nadharia hii inasisitiza kumpa mwanafunzi uwezo wa kuelewa mfumo wa lugha ya kigeni, kisha aendelee yeye mwenyewe kujifunza baada ya kuelewa mfumo huo.

5. Mbinu hii inatambua kuwa mwanafuzni huyu ana akili ya kuweza kujifunza kuhusiana na lugha ile yeye mwenyewe (mtu huzaliwa na uwezo wa kujifunza kutokana na kifaa kilichopo kwenye ubongo KIULU (LAD).

Kwa mantiki hiyo mbinu hii inashadadia mawazo ya Chomsky (1957 na 1968) kwamba umilisi alionao mwenyeji wa lugha ni kama mtambo unaomwezesha kuzalisha maelfu ya tungo mbambali katika lugha yake yaani Umilisi na utendaji (Competence na Performance.

6. Mkabala au mbinu hii inapinga mkabala wa utabia kwamba kujifunza lugha kunatokana na utambuzi na sio tabia ya kurudiarudia yaani uigaji.

7. Kwa kuhitimisha, mbinu hii inazingatia zaidi kumpa mwanafunzi kanuni za msingi za lugha kigeni (lugha anayojifunza na mazoezi yanayoshadadia maana.

## Tafakuri ya Somo

## Zoezi la Somo

1. Kwa kutumia mbinu ya utambuzi onesha namna utakavyokuza stadi za lugha.

2. Fafanua mbinu ya changanyakete kwa kuonesha hatua za kufuata wakati wa kutumia mbinu hii

# Somo la Nne

## Kutumia Mbinu Mahususi Katika Kuwezeshea Stadi za Somo la Kiswahili kwa Darasa La Watu Wazima

### Utangulizi

Katika sura iliyopita tulijifunza kuhusu kuhusu mbinu mahususi za kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili. Katika sura hii tutajikita katika kuangalia maeneo yafuatayo:

- Kufundisha somo la ufahamu
- Kuwezesha stadi za kusikiliza
- Kuwezesha stadi za kuzungumza
- Kuwezesha somo la utungaji
- Kuwezesha stadi za kusoma
- Kuwezesha stadi ya Kuandika

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

▪
▪
▪

## Kufafanua na Kuwezesha Somo la Ufahamu

**4.1.1 Maana ya Ufahamu**

- Ufahamu ni mchakato wa utambuzi wa maudhui yaliyomo katika matini. Ili kufundisha ufahamu wanafunzi wanapewa fursa ya kusoma kimya.
- Ni hali ya kulijua, kutambua na kuelewa jambo kwa usahihi na kuweza kulielezea kwa ufasaha bila kupoteza maana yake ya msingi.

- Ufahamu mara nyingi unahusisha kuona, kusikiliza na kusoma, katika kufanya hivyo mtu hupata maarida fulani kutokana na kile alichokiona, alichokisikia au alichokisoma.

### 4.1.2 Madhumuni ya Kufundisha Ufahamu

- Ni kumwezesha mwanafunzi kuelewa mambo mbalimbali yanayomfikia kwa njia ya lugha pamoja na kukuza ustadi wake katika kuzungumza, kusoma na kuandika.

### 4.1.3 Aina za Ufahamu

**1. Ufahamu wa Kusikiliza**

Ufahamu wa kusikiliza ni ule ambao mhusika anapata taarifa hiyo kwa kusikiliza habari hiyo. Inawezekana kupata habari hiyo kwa kusimuliwa au kusomewa.

Ili kupata habari inayoskilizwa au inayosomwa lazima msikilizaji azingatie mambo yafuatayo:-

i) Kuwa makini kwa kile kinachosimuliwa au kinachosomwa

ii) Kuhusiisha mambo muhimu na habari isimuliwayo

iii) Kujua matamshi ya mzungumzaji

iv) Kubainisha mawazo makuu.

Katika ufahamu wa kusikiliza msikilizaji atalazimika kuwa katika hali ya utulivu, mawazo yake yote yanatakiwa yawe katika mazingira hayo ili neno lisimpite. Hata kama ana matatizo mengi asijali, ikiwezekana amwangalie usoni mtu yule anayemsikiliza, njia hii itamfanya asisahau mawazo.

Katika ufahamu wa kusikiliza, msikilizaji anatakiwa aiweke akili yake yote katika kusikiliza yale anayosomewa au kusimuliwa, hii itamsaidia kujibu maswali kwa usahihi atakapoulizwa. Kwa mfano:- Kuna watu ambao hawamudu kutamka matamshi mfano:- husema ‘laha’ badala ya ‘raha’, au feza badala ya fedha, Ngombe badala ya Ng’ombe. Ukigundua tatizo la matamshi alilonalo mzungumzaji wake itakuwa rahisi kuelewa asemacho.

### 4.1.3 Sababu za Kufundisha Ufahamu

i) Kukuza stadi (kasi, wepesi, ufasaha, ari na ugundizi).

ii) Kukuza ujuzi wa lugha (misamiati, istilahi, miundo, misemo na nahau.

iii) Kukuza maarifa

iv) Kupima ufahamu katika viwango mbalimbali (ufafanuzi, ufupisho)

- Kwa ujumla ufahamu ni uwezo unaojengwa na usikivu na usomaji makini.

### 4.1.4 Sehemu/Aina nyingine za Ufahamu

1. Ufahamu wan nje:
2. Huu ni utambuzi na uelewa wa mambo kutokana na jambo au taarifa iliyo kimuundo, kwa mfano:-

"Ali aliachwa peke yake bila hata rafiki mmoja" baada ya kusikililiza au kusoma taarifa hiyo kuwe na maswali yafuatayo:-

i) Nani aliachwa peke yake?

ii) Aliachwa bila nani?

Majibu ya maswali hayo yapo wazi na yanaonekana katika taarifa husika. Jambo la msiongi ni uwezo wa kukumbuka tu umesikia au kusoma nini?

### 4.1.5 Ufahamu wa Ndani

Ufahamu wa ndani ni utambuzi na uelewa wa mambo utokanao na mazingira au jambo lilivyo likihusishwa na Mazoea aliyonayo msikilizaji au msomaji mwenyewe. Tuchukue mfano ule ule wa Ali aliachwa peke yake bila hata rafiki mmoja. Maswali ya ufahamu huu yatakuwa hivi.

- Kwa sababu gani Ali aliachwa peke yake?
- Katika mazingira gani mtu anaweza kuachwa peke yake?
- Utamsaidiaje Ali baada ya kuachwa peke yake?

Majibu ya maswali hayo hayaonekani kwa nje moja kwa moja. Majibu yanatokana na Mazoea ya maisha ya msikilizaji au msomaji mbali na kumbukumbu ya taarifa, akili yake itampeleka kwenye viwango vya juu zaidi vya fikra.

### 4.1.6 Viwango vya Ufahamu

Kiwango cha ufahamu ni ngazi au kiasi cha fikira ambacho msikilizaji au msomaji anakitumia kupata jibu au ufumbuzi wa aina Fulani viwango vya ufahamu, vina ngazi zake tokay a chini hadi ya juu kabisa kama ifuatavyo:-

1. **Kumbukumbu (recall/memory)**

   Ali aliachwa na nani? na marafiki zake

   - Hapa ni ufahamu wa kumbukumbu jambo Fulani ulilolisikia au kusoma.

2. **Ufafanuzi (paraphrasing)**

   - Maana ya kuachwa nini, Kutengwa, kutekelezwa
   - Ni ufahamu wa kutoa maana ya jambo fulani.

3. **Tafsiri (interpretation** – Ufahamu wa kutafsiri tatizo

   Ali kuachwa peke yake ina uzito gani? Inasikitisha, inahuzunisha, inaleta maswali mengi ya kujiuliza.

4. **Matumizi (Application)**

   Katika tukio gani mtu anaweza kuachwa peke yake?

-	Kifo, ni ufahamu wa kujua/kuelewa chanzo cha tatizo.

5. **Uchambuzi (Analysis)**

   Toa sababu za Ali kuachwa peke yake:-

   Ni ufahamu wa kujua na kuchambua sababu ya tatizo.

6. **Usinyazaji (Synthesis)**

   Tatizo la ali lilikuwa nini? Ufahamu wa kujua mazingira yaliyosababisha tatizo

7. **Tathmini (Evaluation)**

   Unalionaje suala la Ali kuachwa peke yake?

   Ufahamu wa kutathmini ni zito linahitaji msaada wa kina.

8. **Ufumbuzi (problem solving)**

   Utamsaidiaje Ali katika upweke wake?

   Ni ufahamu wa kutatua, kumshauri, kumsaidia kupata ufumbuzi.

9. **Ubunifu (creativity)**

Kilitokea nini baada ya Ali kuachwa peke yake? Ali alihama mji.

Ufahamu wa kupata jibu au ufumbuzi wa tatizo.

### 4.1.7 Jinsi ya Kufundisha Ufahamu

Hatua ya kwanza kabisa ya kufundisha ufahamu ni kuanza kubainisha msamiati uliotumika katika matini hiyo. Hata

hivyo, linalotangulia ni ufundishaji wa uafahanu wa msamiati uliomomo kwenye matini husika. Hatua ya ufundishaji wa msamiati inaweza kujitokeza wakati wowote yaani kabla ya kusoma, wakati wa kusoma na pengine baada ya kusoma. Baadhi ya mbinu zinazoweza kutumika wakati wa kufundisha msamiati ni kama ifuatavyo:

1. Kwa kutumia muktadha au vitu halisi
2. Kwa kutumia picha namichoro ubaoni
3. Kwa kutumia vitedno au matendo
4. Kwa kuhusianisha maneno na visawe vingine.
5. Kwa kufasiri
6. Kwa kutafsiri.

### 4.1.8 Hatua za Kufundisha Msamiati

1. **Andika neon Ubaoni**

Wanafunzi walione na kujua otografia yake na aweze kuhusianisha na matamshi yake na vitu halisi.

2. Waongoze wayasome maneno yote.
3. Waongoze kupata maana kwa kutumia mbinu muafaka kwa ufanisi. Katika kufanikisha hili tengeneza muktadha wa utumizi wake kwa kutumia kisa mafuzno au masimulizi yoyote. Pia epuka kueleza maana ya msamiati kabla ya wanafunzi. Hatua ya kuwapa maana iwe ya mwisho baada ya kushindwa kwa mbinu zote za kumshirikisha.
4. Waongoze wanafunzi watambue maana na kwa kuwauliza maswali kama yanayolengwa kutoa maana ya msamiati.

5. Waongoze wanafunzi waandika maana ya msammiati ubaoni au daftarini.
6. Rudia hatua hizo kwa maneno yote kisha uwaongoze uwaongoze wanafunzi wasome kimya habari au matini ya ufahamu.
7. Waongoze wajibu maswali baada ya kusoma.

## Kufafanua na Kuwezesha Somo la Utungaji

**Utungaji unatokana na kitenzi tunga**

Kitenzi tunga maana yake ni kuweka mpangilio wa mawazo au habari katika maandishi au mazungumzo ili yaeleze jambo Fulani au jambo lililokusudiwa.

**Maana ya Kutunga**

Ni kuunda hoja au mawazo kwa kutumia fikra, kuyapanga mawazo katika mtiririko unaofaa na kugha inayoeleweka kuyawasilisha mawazo hayo ili yatoe ujumbe uliokusudiwa.

**Utungaji hufanyika kwa njia mbalimbali**

1. Mazungumzo/masimulizi
2. Maandishi.

**Dhima ya Utungaji**

1. utungaji hiwezesha watu kutoa mawazo au maoni kwa njia ya maandishi au mazungumzo, maoni hayo yanaweza kuwa maoni ya mtu binafsi au ya watu wengine.

2. Utungaji huwezesha utungaji wa lugha fasaha, sanifu na uweszo wa kujieleza kwa njia ya maandishi au mazungumzo.

3. Utungaji husaidia kuweka mpangilio mzuri wa mawazo kimtiririko na matumizi sahihi na fasaha ya lugha na kufuata kanuni za uandishi.

4. Utungaji huwezesha suala la ubunifu katika masimulizi au maandishi ya kazi yoyote ile ya kubuni, hususan kazi za fasihi.

5. Utungaji huweza kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu maisha yetu ya kila siku kupitia njia ya utungaji, watu hupata taarifa kuhusu vitu mbalimbali vinavyozunguka maisha yao ya kila siku.

6. Utungaji hutumika kuelimisha, kukosoa na hata kuonya, maandishi au mazungumzo yanayotokana na utungaji huweza kuaksi (kuelezea) hali halizi ya maisha ya jamii, na hivyo ikawa ni kama kioo cha kujitazama na kujirekebisha.

7. Utungaji hususan unaotokana na kazi za fasihi hutumika kubirudisha jamii. Hadithi na tanzu nyingine za fasihi zinazotokana na utungaji huburudisha, kna kufurahisha jamii.

8. Utungaji hutumika kukuza lugha kwa njia ya mazungumzo au maandishi. Mzungumzaji na msikilizaji hupata ufundi wa kujieleza zaidi kupitia njia ya utungaji.

**Kanuni za Utungaji Bora**

Utungaji bora ni lazima uzingatie kanuni zifuatazo:-

i) Matumizi mazuri ya nyakati, mfano wakati uliopita, wakati ujao na wakati uliopo au hali timilifu.

ii) Matumizi mazuri ya lugha fasaha (lugha inayoeleweka)

iii) Mpango mzuri wa mawazo na mantiki, yaani kutochanganya mawazo, kutorudia mawazo au kutosahau mawazo.

iv) Matumizi bora ya vituo na alama mbalimbali kama vile mkato, (,), nukta (.), nukta mkato (;), nukta mbili au nukta pacha (:).

v) Matumizi bora ya kufuata kanuni za sarufi ya lugha inayohusika.

vi) Utungaji bora hugawanyika katika sehemu kuu tatu:-

- Mwanzo (utangulizi) mtungaji atoe maelezo mafupi kuhusiana na habari anayotaka kuitunga.
- Kati (habari yenyewe)
- Mwisho hutoa majumuisho yaliyojadiliwa katika habari yenyewe

vii) Uwe wa kueleweka kwa wazi, mtungaji aepuke utata

viii) Uwe na mvuto, yaani uwe wa kuvutia na kusisimua.

ix) Uwe na mifano bora.

**Mambo Muhimu ya Kuzingatia katika Utungaji**

1 Maudhui: Jambo au ujumbe au wazo linalozungumziwa au linalojadiliwa.

2 Lengo la maudhui hayo, mfano kuelimisha, kufundisha, kuonya, kuburudisha n.k.

3 Lugha, inaweza kwa mazungumzo ya maandishi, ni lazima iwe na maneno yenye utoshelevu na awe fasaha.

4 Mpangilio wa uwasilishaji mpango na utaratibu wa maelezo, masimulizi na maandishi.

5 Hadhira – watu wa kusikiliza au kusoma habari iliyotungwa.

**Matumizi ya Vituo na alama Mbalimbali katika Utungaji na uandishi**

1. Mkato (,) au koma alama hii hutumika:-

(a) Kuweka pumziko fupi katika sentensi mfano:-

Tulipofika sokoni, tulinunua samaki.

(b) Kutenga maneno yaliyo katika orodha mfano:-

Ukifika sokoni nunua dagaa, ndizi, mkaa na unga.

(c) Hutumika badala ya kiunganishi katika sentensi mfano:-

Umoja ni nguvu lakini, utengano ni dhaifu

Umoja ni nguvu utengano ni dhaifu.

(d) Hutumika kabla ya alama za mtajo:-

Mfano:- John alimwambia, “Nakupenda kama pipi.

**2. Nukta (.) Alama hii hutumika**

(a) Kukamilisha sentensi mfano – mtoto wangu amefika.

(b) Kuonyesha ufupisho wa maneno kama vile kwa mfano:-

K.V - kama vile

K.M - Kwa mfano

N.K - Na kadhalika

S.L.P - Sanduku la Posta

**(c) Nukta pacha na kistari (:)**

Alama hii hutumia kuashiria sentensi fupi fupi zuizo katika hali ya mfululizo wa orodha mfano:- Madhumuni ya kuanzisha kikundi hiki ni haya:-

(a) Kupiga vita ukimwi

(b) Kupambana na umasikini

(c) Kuhimiza utunzaji wa mazingira

**4. Nukta mkato (;),**

Alama hii hutumika kuunga sentensi mbili zinazoweza kusimama zenyewe bila kutumia kiunganishi.

**5. Nukta mbili au nukta pacha (:)**

Alama hii hutumika kutaja maneno yaliyo katika orodha mfano:-

(a) Niletee vitu hivi: wino, karatasi, kalamu na kiti.

(b) Ninunulie matunda haya: embe, nduimu, chungwa na ndizi.

**6. Alama ya kushangaa (!)**

Hutumika kabla ya neno au semi wa kushangaa au kushtuka, Huweza kuonyesha uchungu au huzuni mfano:-

(i) Lo! Maskini ndugu yangu amefariki

(ii) Kumbe alikuwa mwizi wa mitumba.

**7. Alama ya kuuliza (?)**

Hutumika kuuliza swali

Mfano: Je utafika saa ngapi?

Unasemaje?

**8. Mabano ( )**

Hutumika kuonyesha maana ya ziada katika sentensi.

Mfano:- Nchi yetu (Tanzania) tunaipenda sana.

**9. Kistari (-)**

(i) Hutumika kuonyesha neno bado linaendelea linapofikia ukingoni mwa karatasi.

(ii) Hutumika kuunga maneno au kujenga neno moja, mtindo huu unajitokeza katika maneno yenye asili ya kigeni. Mfano:-

- Idd-el-fitri
- Dar –es-Salaam

**10. Alama za mtajo (“ ”)**

Hutumika katika kukariri maneno aliyosema au aliyoandika mtu mwingine.

**11. Ritifaa ( ’ )**

(a) Hutumika kutofautisha ng na ng’ katika baadhi ya maneno kama vile ng’ombe, ng’arisha, ng’ang’ania, ng’ambo, ng’amua n.k.

(b) Huonyesha kuwa herufi fulani imeachwa mfano:- N’ mechelewa, N’kuvute n.k.

**12. Nukta Katishi (………)**

(a) Hutumika kubainisha mdokezo

Mfano:- Nampenda yule mrembo lakini ………………

(b) Hutumika kuonyesha kuwa kuna maneno yaliyotangulia katika utungo mfano:- ………… fika ofisini mara moja.

**13. Matumizi ya Herufi kubwa**

(a) Hutumika kila mwanzo wa sentensi

(b) Hutumika baada ya alama hizi (.), (?), (!), n.k.

(c) Hutumika kutaja majina ya pekee

Mfano:- majina ya watu, Mji, Nchi, bara n.k.

## Kufafanua na Kuwezesha Somo Ufahamu wa Kusoma

- Ufahamu wa kusoma ni kuzingatia maana ya neon, sentensi na habari yote, msomaji lazima aweze kutambua mpangilio wa herufi, maneno, na tarakimu na kuzitofautisha.
- Ufahamu wa kusoma ni ule uelewa unaopatikana kwa njia ya:-

i) Kusoma kwa sauti

ii) Kusoma kwa haraka na kimya

iii) Kusoma kwa makini

- Katika ufahamu wa kusoma, msomaji anahitaji kutambua mambo yafuatayo:-

i) Kubainisha mawazo makuu

- Abainishe mawazo au dhamira zinazojadiliwa na mwandishi wa habari anayosoma.

ii) Kubainisha maana ya maneno na misemo

Katika hapa mara nyingi kuna maneno magumu zipo njia za kupata maana ya neno au maneno katika habari, ni kwa kutumia kamusi.

iii) Kwa kuzingatia muktadha (mazingira) ambamo neno au maneno haya yametumika msomaji hulazimika kusoma kifungu cha habari hadi akielewe, baadaye huangalia neno linalohusika akizingatia lilivyotumika.

iv) Hapa atapata maana ya neno kama lilivyotumika kulingana na habari kwa kuwa neno moja huweza kuwa na maana nyingi.

### 4.3.1 Jinsi ya Kujibu Maswali Uliyosoma

i) Soma makala inayohusika

ii) Soma maswali uliyoulizwa ili kujua nini kinachotakiwa

iii) Unatakiwa kurudia kusoma makala yote hapa, utasoma kwa makini huku ukijitahidi kupata mawazo muhimu ya majibu ya maswali yaliyoulizwa.

iv) Katika hatua hii, msomaji anaweza kutumia kalamu ya risasi kuweka alama katika sehemu ile unayodhani ni jibu sahihi.

v) Baada ya kusoma makala hiyo na kuweka alama majibu yako sasa msomaji anaweza kujibu maswali yanayohusika, usikiuke maagizo.

### 4.3.2 Aina za Maswali katika ufahamu wa kusoma

1. Maswali mafupi
2. Maswali marefu

1. **Maswali mafupi**
   - Ni yale ya kuchagua jibu sahihi, katika majibu kadhaa yaliyotolewa.
   - Maswali ya kujaza kwenye nafasi iliyoachwa wazi
   - Maswali ya kuonyesha ni zipi kati ya hoja zilizotolewa ni sahihi na zipi siyo sahihi.
   - Maswali ya kuainisha 'A' na 'B' ili yalete maana.
2. **Maswali Marefu**
   - Ni yale yanayohitaji kujibiwa kwa maelezo ya sentensi zenye hoja kadhaa kwa kujadili au kutoka maoni.
   - Kuandika habari isiyozidi maneno mia mbili n.k

### 4.3.3 Kufafanua na Kuwezesha Stadi za Kusoma

**Ufahamu wa kusoma**

Ni ule welewa unaopatijkana kwa njia ya kusoma kwa makini maandishi fulani mfano kitabu, gazeti au kipeperushi.

**Usomaji upo wa aina kuu mbili nazo ni:-**

a) Kusoma kwa sauti

b) Kusoma kwa haraka na kimya

**Mambo ya kuzingatia wakati wa kusoma**

**a) Kuwa mtulivu**

- Kuelekeza fikra zote kwenye kile anachokisoma

- Kuweza kuielewa vizuri mada kuanzia utangulizi wake, kiini, hitimisho

na uhusiano wa mada na maswali yaliyoulizwa.

**b) Kusoma kwa makini**

- Msomaji huweza kuisoma habari hyote kwa ukamilifu bila kuruka baadhi ya aya.

**c) Kuelewa swali**

i) Eleza dhima ya fasihi

ii) Waandishi wa kazi za fasihi ni wakombozi wa jamii, jadili kauli hii.

## Kufafanua na Kuwezesha Stadi za Kusikiliza

### 4.4.1 Dhana ya Kusikiliza

**Kusikiliza ni nini?**

Kusikiliza ni hali ya kupokea na kufasili ujumbe kutoka kwa mzungimzaji. Hii ndiyo stadi ya kwajza ya kimsingi. Ili kuzikuza stadi zile zingine za lugha, mtu anapaswa kusikiliza yanayosemwa. Hii diyo sababu, ikiwa mtu hawezi kusikiliza ipasavyo, anaishia kuwa na matatizo ya kuongea. Ikimbukwe kwamba kusikiliza bdiyo msingi wa stadi zingine zote. Kwa mantiki hii, makosa yote yanayotokea kwenye lugha andishi, chanzo chake kinatokana na lugha ya zungumzi.

Stadi ya kusikiliza hujulikana kama ufahamu sikizizi ambao ni ule ufahamu anaoupata mtu kwa kusikiliza habari fulani inawezekana kwa kusimuliwa au kusomewa. Ufahamu sikizi huwa na madhumuni ya kusikiliza ujumbe, kuudhibiti na kuufasili kwa minajili ya kuitikia.

Stadi ya kusikiliza huunganisha watu wawili, anayezungumza na mpokezi kwani inahusu upashaji habari, upokeaji na ufasiri wa ujumbe uliotolewa kwa msimbo wa sauti.

### 4.4.2 Mambo ya Kuzingatia katika Kujibu Maswali ya Ufahamu na Kusikiliza

1. Kubaini mawazo makuu

Ni wajibu wa msomaji au msikilizaji (hadhira) kutambua mawazo ya mwandishi au msimuliaji. Kwa mfano: Wanafunzi wa shule yetu ni wakarimu na wachapakazi hodari.

Katika kubaini mawazo makuu, yafuatayo yaweza kuwa mawazo makuu, Ukarimu na uchapakazi

2. **Kubaini maana ya maneno na misemo**

- Kubaini maneno magumu:  Kutafuta kwenye kamusi.

3. **Kusikiliza kwa utulivu**

Kuelekeza fikra zake kwenye maelezo yanayotolewa.

### 4.4.3 Malengo ya kufundisha kusikiliza

(a) Kutofautisha na kutafsiri/kufasiri kilichoelezwa

(b) Kutambua matamshi ya maneno/viimbo na mikazo

(c) Kutambua alama mbalimbali za lugha wakati wa kuzungumza mfano: Vitendo (gesture)

(d) Kuwasaidia wanafunzi wapatre uelewa wa jumla wa mawasiliano ya kimazungumzo.

### 4.4.4 Mbinu za kufundishia Stadi ya Kusikiliza

- Ngonjera
- Nyimbo
- Matangazo redioni/runingani na vinasa sauti
- Maigizo
- Hadithi n.k

Ni vema kukumbuka kuwa ufundishapo stadi ya kusikiliza unafundisha pia kuzungumza.

### 4.4.5 Hatua za kufundisha stadi ya kusikiliza:-

1. Soma matini/weka rekodi au kinasa sauti
2. Soma matini kwa sauti au weka rekodi kwa mara ya pili
3. Waongoze wanafunzi kubaini misamiati waliyoisikiliza kasha ufundishe kwa kufuata hatua zote
4. Waulize maswali ili wayajibu kwa mdomo au kwa kuandika
5. Waweke kwenye vikundi ili walinganishe majibu yao kama wameandika
6. Waongoze wayawasilishe mbele ya wenzao darasani
7. Waulize maswali zaidi ya jumla na mahususi kwa ajili ya ufahamu.

Ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi anakuza stadi ya kusilikiza, mwalimu ana wajibu wa kumuelekeza katika misingi bora ya

kusikiliza lugha ya Kiswahili inapozungumzwa na wengine ilia pate kuelewa yanayosemwa kwa urahisi.

Pia, mwalimu ana wajibvu wa kukuza usikizi makini wa mwanafunzi ili aweze kucghuja sauti mbalimbali za lugha ya Kiswahili zinapotamkwa.

## 4.5 Kuwezesha Stadi za Kuzungumza

Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2012: 239) stadi ya kuzungumza hujlikana kama stadi ya kuongea. Kuongea ni kitendo kinachohusisha watu wawili au zaidi ambapo wahusika ni wasikilizaji na wakati huo huo wazungumzaji ambao huchangia kwa kila mmoja kutoa maoni yake. Kimsingi kuongea kuzungumza ni fani ya lugha ambayo kwayo ujumbe wa mzungumzaji huwasilishwa kwa anayesikiliza kupitia msimbo wa sauti.

### 4.5.1 Umuhimu wa Stadi za Kusikiliza na Kuongea

Kuna haja ya kuzingatia stadi ya kusilikiza na kuzungumza katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa sababu makosa mengi ya maandishi chimbuko lake ni katika usikilizaji, mazungumzo na matamshi mabaya, aidha makosa mengi yana mizizi yake kutoka katika lugha mama ambayo huwa na athari kubwa kwa wanafunzi kwa sababu wanafunzi huanza kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

### 4.5.2 Shabaha za kuimarisha stadi za kusikiliza na kuzungumza

- Kukuza kipawa cha wanafunzi cha kusikiliza na kupokea kilichosemwa.
- Kuwawezesha wanafunzi kuchuja na kubainsha sauti za lugha ya Kiswahili.
- Kuimarisha usikilizaji li wawe na uwezo wa kutathmini mambo.
- Kusikiliza ili waweze kutathmini ujumbe wanaosikiliza
- Kujieleza kwa ufasaha
- Kupanga maneno na tungo kwa kuzingatia Kiswahili sanifu.

- Kuwa na uwezo wa kuzungumza kwa ukakamavu na ujasiri mbele ya wenzao.
- Kuweza kuzungumza kwa mtiririko na mfululizo.
- Kusikiliza na kuitikia maagizo
- Kupambanua athari zinazotokana na lugha mama na jinsi ya kukabiliana na athari husika kimatamshi na kisarufi.

### 4.5.3 Matatizo yanayoathiri za Kusikiliza na Kuzungumza

- Ukosefu wa hamu ya kujifunza
- Ugumu wa dhana au mada zinazofafanuliwa na mwalimu,
- Uchovu wa mwili na akili ambao unaweza kutokana na njaa.
- Mwalimu hujitia ubingwa katika matamshi na matumizi yay a msamiati mgumu kwa wanafunzi.
- Mtiririko mbaya wa mawazo kwa uoande wa mwalimu.

### 4.5.4 Jinsi ya kutatua Vikwazo vinayoathiri Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza

- Mwalimu kuwahamasisha na kuwamotisha wanafunzi kwa kutumia mbinu mwafaka za ufundishaji.
- Kuchuja na kuchagua mada ambazo ni sahili na zinazozoana na kiwango cha wanafunzi. Mwalimu anahitaji kufahamu tofauti za wanafunzi wa kidato cha kwanza, pili, tatu na cha nne ili kuzingatia mada zifaazo katika kila kiwango.
- Mwalimu kufundisha mada ambazo zinaenda sambamba na tajiriba za wanafunzi wake.
- Mwalimu kutanguliza somo kwa kudondoa vidokezo vya yale anayotaka kufundisha wanafunzi wake.

**Jinsi ya kutatua Tatizo la Athari ya Lugha Mama**

(i) Mwalimu kubainisha sauti tatanishi, kigezo kikiwa ni mazingira ya wanafunzi.

(ii) Mwalimu kuongeza juhudi za utamkaji wa sauti tatanishi kwa ufasaha ili kuwa kielelezo kwa wanafuzni wake.

(iii) Pia kuandaa mafunzo mengi ya imla ili kukuza usikilizaji miongoni mwa wanafunzi wake.

### 4.5.5 Jinsi ya kutatua tatizo la kusikiliza na Kuzungumza kwa Wanafunzi wenye ulemavu

Walimu kuwashauri wazazi wa wanafunzi husika kuwatembelea wataalam wanaoshughulikia matatizo ya usikizi.

Wanafunzi wenye tatizo la usikilizaji hafifu kuketi karibu na mwalimu.

Mwalimu kuzungumza kwa sauti ya juu yenye nguvu ili walio na matatizo waweze kumsikia.

### 4.5.6 Jinsi ya Kutatua Tatizo la Fikra Potovu Miongoni mwa Wanafunzi kuwa lugha ya Kiswahili ni Rahisi pia Mielekeo hasi ya wasomi dhidi ya Lugha ya Kiswahili

Mwalimu kuwaonyesha wanafunzi wake umuhimu wa lugha ya Kiswahili kama lugha taifa, biashara na kimataifa.

Kujenga mazingira ambayo yanawamotisha wanafunzi katika stadi za kusikiliza na kuongea anapofundisha.

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba hatuwezi kutenganisha stadi za kusikiliza na kuongea kwa sababu stadi hizi mbili hubadilishana nafasi papo kwa papo katika mchakato wa kuwasiliana.

## Tafakuri ya Somo

## Zoezi la Somo

1. Ukiwa wewe ni mwalimu wa elimu ya watu wazima eleza namna utakavyowasaidia wanafunzi wenye matatizo ya kusikiliza na kuzungumza wakati wa kujifunza somo la Kiswahili.

# Somo la Tano

## Kuandaa Zana za Kuwezeshea Somo la Kswahili kwa Darasa la Watu Wazima

### Utangulizi

Katika sura iliyopita tulijifunza jinsi mbinu mahususi zinavyoweza kutumika katika kuwezeshea stadi za somo la Kiswahili. Katika sura hii tutajifunza kuandaa zana za kuwezeshea somo la Kiswahili kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

- Kuelezea maana ya zana za kuwezeshea
- Kubainisha makundi ya zana za kuwezeshea
- Kufafanua faida za zana za kuwezeshea
- Kufafanua sifa za zana za kuwezeshea
- Kufaragua zana za kuwezeshea

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- 
- 

### Dhana ya Zana za Kuwezeshea

**Zana a Kuwezesha**

Maana ya zana za kuwezeshea

Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi 2013: 203) wanafafanua zana kama vifaa mbalimbali ambavyo mwalimu hutumia ili kuwasilisha na kufaulisha funzo/ mada husika kwa wanafunzi wake. Zana ni muhimu kwa sababu huwafanya wanafunzi waelewe kwa urahisi na kwa haraka tofauti na ikiwa mwalimu havitumii. Kwa ujumla, zana ni kitu chochote kinachopangwa/kuandaliwa na kutumika katika kuinua kiwango cha Elimu.

Zana za Kufundishia zaweza kuwa za ziada au unganishi.

Zana za ziada ni zile ambazo zinazomsaidia mwalimu kuchapua somo lake na hazitoi fursa ya kujifunza kwa vitendo yale mambo anayojifunza, bali mwanafunzi hubaki kusikiliza tu. Mfano (redio, tepu rekoda na santuri).

Wakati zana unganishi ni zile zenye msaada mkubwa wakati wa ufundishaji, zana unganishi hazimsaidii mwanafunzi katika kujifunza tu bali zinamsaidia mwanafunzi kufanya kwa vitendo yale anayojifunza. Mfano, vitu halisi, chati, ramani, picha na maabara).

## Aina mbalimbali za Zana za Kujifunzia

Zana za kufundishia zinaweza kuanishwa katika mafungu mawili makuu ambayo ni:

**(i) Vifaa halisi**

Hizi ni zana ambazo ziko katika maumbo halisi na hazibadilsihwa kwa vyovyote vile. Ni vitu ambavyo vinaweza kubebwa hadi darasani, Kwa mfano matunda, vyombo vya kupakulia, mavazi mbalimbali n.k. Kutokana na zana halisi Mwanafunzi anajifunza kwa udadisi, kuchunguza na kugundua, pia vitu halisi vinampa mwanafunzi nafasi kubwa ya kujifunza kwa vitendo na kutumia milango mingi ya fahamu kwa wakati mmoja, mfano meza, kiti n.k.

**(ii)Vifaa vibadala Maumbo/Modeli (Vifaa Bandia)**

Hivi ni zana ambazo huchukua nafasi ya vifaa halisi na mabvy haviwezi kubebwa darasani. Vifaa hivi vinaweza kuwasilishwakwachati. Grafu, ramani, michoro, picha, chati, sanamu, mabango na vinyago. Pia zana za kidigitali zikiwemo televisheni, Video sinema, radio, santuri na tepu rekoda. Kwa mfano, televisheni inachangia katika kuonyesha vitu vilivyo kwa hali hii kuna ukweli ndani ya televisheni. Pia televisheni inamwezesha mwanafunzi kusikia na kuona matendo wakati ule ule yanapofanyika.

Nafasi ya vifaa mabadala / Bandia/Maumbo (modeli) ni kuwa hutumika pale ambapo kunakuwa na ukosefu wa vitu halisi, maumbo, vitu bandia huchukuwa nafasi ya pili, mwanafunzi anapata kuona, kusikia, kuhisi kana kwamba anatumia vitu halisi,

bandia ni mfano wa vitu halizi hivyo huchangia kiasi fulani cha ukweli mfano picha za vitu mbalimbali (samba, mtu, sungura n.k). Umuhimu wa chati, picha mabango, grafu na ramani ni kuwa hutoa mwasiliano ya kuona tu. Mwanafunzi anajifunza kwa kutumia macho yake na viungo vingine vya ufahamu. Umuhimu wa redio, santuri, tepu rekoda ni kuwa zana hizi humsaidia mwanafunzi kujifunza kwa kusikia vipindi maalumu, hutayarishwa kwa ajili ya shule au wanafunzi wanaosoma kwa masafa (Distance Education).

## Makundi ya Zana za Kuwezesha

Zana za kuwezesha zimegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni:-

i) Zana masikizi ambazo ni filimbi, radio, kanda za sauti na kinasa sauti.

ii) Zana maono ambazo ni grafu, picha, mabango na ramani

iii) Zana masikizi maono ambazo ni televisheni na sinema.

## Sifa za Zana za Kuwezeshea

i) Zana au vifaa vya kufundishia view na umuhimu na maana katika kufundisha na kuwasilisha maana iliyokusudiwa.

ii) Zana au kifaa kisiwe na taarifa za ziada isiyohitajika katika somo husika ili kumtompoteza mwanafunzi.

iii) Zana au kifaa kisiwe na makosa au upotofu wa taarifa iliyomo au inayopaswa kuwasilishwa.

iv) Kifaa kiwe cha kuvuitia ili kiweze kuvuta ndhari ya wanfunzi yaani kiwe na muonekano mzuri.

v) Ubunifu wa zana za kufundishia utilie ya mwanafunzi maanani suala la mazingira

vi) Kifaa/zana inayotumiwa katika kufundishia darasani kisimsababishie mwanafunzi madhara yoyote.

vii) Vifaa viwe na uwezo wa kuhifadhika

viii) Vifaa vinavyobuniwa vitilei maanani gharama ya utengenezaji’

ix) Ziwe wazi na zieleweke/zitambulike

x) Zimsaidie mwanafunzi kufanya kazi kwa vitendo

xi) Zionyeshe uhalisia katiaka kujifunza

xii) Ziinue na kukuza kiwango cha kujifunza

xiii) Ziwe na uhusiano na mada husika

## Faida ya Zana za Kuwezeshea

i) Zinamsaidia mlengwa/mwanafunzi kuona, kusikia uhalisia wa zana husika

ii) Humsaidia mwezeshaji/mwalimu kuandaa zana za kujifunzia na kufundisha

iii) Humsaidia mwezeshaji kuandaa zana kulingana na uwezo wa wanafunzi

iv) Zinamsaidia mwanafunzi/mwalimu kufanya kwa vitrendo yale anayojifunza au kufundishia

v) Zinakuza na kuinua kiwango cha kujifunza

vi) Zinasaidia kupima ubora na udhaifu katika ufundishaji.

## 5.6 Umuhimu au Manufaa ya zana za Kufundishia na Kuwezeshea

1. Vifaa hurahisisha maelezo ya mwalimu
2. Kuokoa muda wa kueleza mambo
3. Vifaa huleta uwazi katika somo;
4. Vifaa humsaidia mwanafunzi kuelewa vizuri zaidi.
5. Zana/vifaa hupitisha maarifa kwa wanfunzi kwa urahisi.
6. Zana/vifaa hukuza kipawa cha kuhifadhi mambo yaani wanafunzi hukumbuka walichofundishwa kwa urahisi.
7. Zana zikiwa na muonekano mzuri, hufurahisha, kuburudisha na kuwafurahisha wanafunzi wakati wa kuwasilisha somo.
8. Wanafunzi kupitia matumizi ya vifaa hujifunza utendaji zaidi ya kusikiliza.
9. Ni jambo la msingi kukumbuka kwamba kila somo linapaswa kuandaliwa zana na zana hizi zinapaswa kutundikwa na kutumika wakati muafaka tu ili zana isiwe chanzo cha kuwakanganya wanafunzi.

## Tafakuri ya Somo

## Zoezi la Somo

1. Fafanua vigezo vya uteuzi wa mbinu za kuwezeshea somo la Kiswahili.

2. Eleza umuhimu wa zana za kuwezeshea somo la Kiswahili.

# Somo la Sita

## Kupima Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili

### Utangulizi

Katika somo lililopita tulijifunza zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kwa undani na kwa ufasaha. Katika sura hii tutajifunza kuhusu somo la upimaji wa wanafunzi katika ujifunzaji kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

- Kueleza maana ya upimaji
- Kubainisha aina za upimaji
- Kuandaa zana za upimaji
- Kufafanua ubora na udhaifu wa zana za upimaji
- Kufafanua faida za upimaji

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

▪

▪

### Maana ya Upimaji/Tathmini

Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2013:189-190) upimaji ni sehemu muhimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kwa ni humfanya mwalimu kuwa tayari anapojiuliza maswali mbalimbali baada ya kila hatua ya uwasilishaji wa somo lake. Majibu ya maswali anayojiuliza katika kila hatua yanamkumbusha ikiwa malengo yake mahususi yameashaafikiwa au la. Mwasali haya ni kigezo muhimu cha kumwezesha mwalimu aweze kujua iwapo shabaha zake mahususi zimeafikiwa au la.

Hivyo basi, upimaji hurejelea kitendo cha kufanya tathmini katika tendo la ujifunzaji na ujifunzwaji ili kupata ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa na stadi alizofundishwa.

Mwalimu anapotathmini wanafunzi wake, anaweza kufukia uamuzi wa kutathmini mbinu za ufundishaji, zana anazozitumia ili

kuboresha uelewa wa wanafunzi wake na utendakazi wake. Upimaji unaweza kujitokeza kwa namna mbili, yani upimaji endelezi na upimaji wa mwisho wa muhula.

## Aina za Upimaji way Somo la Kiswahili

### 6.2.1 Upimaji wa Awali

Huu hufanyika mwanzoni kabisa ili kupima uwezo, ujuzi, na uelewa wa mwanafunzi.

### 6.2.2 Upimaji Endelevu/ Endelezi

Upimaji huu hufanyika wakati wa tendo la ujifunzaji likiendelea. Upimaji huu lengo lake kuu ni kuangalia endapo malengo maudhui yaliyokusudiwa yanawafikia walengwa. Katika aina hii ya upimaji mwalimu anaweza kuwatathmini wanafunzi wake ama kwa juma ama kwa kila mwezi. Mazoezi mbalimbali yanayoweza kupima stadi mbalimbali za lugha kama kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika yanaweza kuandaliwa ndani ya juma moja au mwezi mmoja.

Wanjala na Kavoi 2013:217) wameanisha manufaa ya kuweka kumbukumbu za tathmini endezi kama ifuatavyo:

(i) Huonyesha maendeleo ya wanfunzi na humwezesha mwalimu kutoa ushauri kwa wanafunzi wake

(ii) Kupitia hati hii, mwalimu anaweza kubainisha wanafunzi walio na shida na kuwashughulikia.

(iii) Hati hii ni ushahidi kamili wa kuwa mwalimu amekuwa akifanya kazi iwapo wakuu wake au maafisa wa elimu wanashaka na utendakazi wake.

(iv) Kumbukumbu ya tathmini endelezi humpatia mzazi na mwalimu nafasi ya jinsi wanavyoweza kuasaidia ili kuboresha matokeo ya mwanafunzi husika.

### 6.2.3 Upimaji Gunduzi

Upimaji huu hufanyika ili kujua au kugundua udhaifu alionao mwanafunzi katika tendo zima la ujifunzaji.

### 6.2.4 Upimaji Tamati/ Mwisho wa Muhula

Upimaji huu hufanyika mwishoni mwa mafunzo mara nyingi hutolewa na tuzo; mfano Cheti n.k. Katika upimaji huu, mwalimu anaweza kuwatathmini wanafunzi katikati ya muhula na mwisho wa muhula na kuunganisha alama zote kwa pamoja ili baadaye aziunganishe alama za upimaji endelezi ambazo hujumuisha majaribio mbalimbali. Mwalimu anashauriwa kuwatathmini wanafunzi wake kila mara.

**Umuhimu wa Upimaji**

1. Kupima uwezo wa mwanafunzi na kuelewa alichofundishwa.
2. Kupima shabaha za mwalimu alizojiwekea mwanzoni mwa somo.
3. Kumwezesha mwalimu kufikia uamuzi ikiwa baadhi ya wanafunzi wanahitaji usaidizi.
4. Humpatia mwalimu nafasi ya kukadiria maendeleo maendeleo ya wanafunzi.
5. Upimaji humwezesha mwalimu kujitathmini na kukadiria iwapo wanafunzi wake walielewa alichokifundisha au la.
6. Upimaji huwa ni mizani kwa mwalimu ambayo humwezesha mwalimu kufanya maamuzi juu ya ikiwa atarudia hatua ya kwanza kabla hajaendelea na inayofuata.
7. Upimaji pia humwezesha mwalimu kuamua ikiwa baadhi ya wanafunzi wanahitaji mafunzo ya ziada au la.
8. Kutokana na umuhimu wa upimaji, sentensi kuhusu upimaji inavyopaswa kuendeshwa na kutolewa katika kielelezo cha maazimio katika safu ya upimaji. Safu ya upimaji hupambanua maswali ambayo mwalimu hujiuliza ili kukadiria kiwango cha uelewa wa wanafunzi baada ya kila hatua ya somo.

## Mbinu na Zana za upimaji (Vifaa vya Upimaji)

**Vifaa vya Upimaji**

**i) Maswali**

Mara nyingi zana hii hutumika darasani pale mwezeshaji/mwalimu anapowauliza maswali wanafunzi kulingana na mada anayofundisha.

**ii) Majaribio**

Zana hii hutumika kuwapima wanafunzi pale mwalimu anapomaliza kufundisha mada yake ili kuwapima wanafunzi uelewa wao.

**iii) Mazoezi**

Zana hii ya upimaji hufanyika wakati mwalimu au mwezeshaji anafundisha na baada ya kufundisha mada husika.

**iv) Mitihani:** Zana hii ya upimaji hutumika mara nyingi mwishoni pale ambapo tayari wanafunzi wamemaliza mada zote (kwa muhula fulani (mwaka husika).

## Tafakuri ya Somo

## Zoezi la Somo

1. Fafanua zana za upimaji na uoneshe namna ambavyo utazitumia katika kuwapima wanafunzi watu wazima.
2. Eleza umuhimu wa upimaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi watu wazima.

# Maswali ya Marudio na Majadiliano

1. Onesha uhusiano uliopo kati ya mbinu mahususi za kuwezesha somo la lugha na nadharia za ujifunzaji lugha.

2. Onyesha mchango wa akili katika kujifunza lugha kwa kuzingatia misingi ya nadharia za ujifunzaji na mtazamo wa Chomsky.

3. "Chomsky anaeleza kuwa mtoto anajifunza lugha kwa urahisi na ufanisi mkubwa kuliko mtu mzima." Jadili usemi huu kwa kuuonyesha kipindi maalum ambacho mtoto mtoto hueza kuamilia na kujifunza lugha kwa urahisi na uoneshe uoneshe wataalam waliozungumzia kuhusu kipindi maalum cha kuamili lugha.

4. Tathmini mawazo ya Chomsky kuhusu ujifunzaji lugha kwa kuzingatia misingi ya na mawazo makuu ya nadharia hii kisha uonyeshe ubora na udhaifu wa nadharia yake.

   Kuna umuhimu gani wa walimu wanaofundisha lugha kuwa na uelewa wa nadharia na mbinu mbalimbali za kujifunzia lugha? Kama ndivyo, uelewa wako kuhusu umuhimu wa mwalimu wa lugha kujifunza nadharia za ujifunzaji lugha.

5. Chagua mada ya somo lolote kisha uonyeshe jinsi ufundishaji wake unavyohusiana na misingi ya nadharia zozote mbili za ujifunzaji lugha.

6. Fafanua kwa ufupi misingi mikuu ya nadharia (4) nne za ujifunzaji lugha ulizojifunza darasani kwa kuonyesha waasisi wake.

7. Onesha uhusiano uliopo kati ya mbinu mahususi za kuwezeshea somo la lugha na jinsi utakavyowezesha stadi za lugha.

8. Onyesha ubora na udhaifu wa kila mbinu mahususi ya kuwezeshea somo la lugha kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

   (a) Eleza kwa ufupi misingi yay a mbinu hiyo.

   (b) Onyesha ubora

   (c) Onesha udhaifu wa mbinu hiyo

   (d) Taja na eleza mada zinazoweza kufundishwa kwa mbinu hizo.

**9.** Kufundisha kanuni za lugha katika hatua za awali za kufundisha miundo ya lugha ni "usumbufu" na kwamba kitendo hichi kinakiuka misingi ya nadharia tete za baadhi ya nadharia za za kufundishia na kujifunzia lugha. Jadili usemi huu kwa kuzingatia mbinu na nadharia za kufundishia lugha.

**10.** Mwalimu yoyote wa lugha lazima awe makini katika kuzitambua na kuzirekebisha dosari mbalimbali ambazo huweza kujitokeza katika mchakato mzima wa ujifunzaji lugha. Jadili usemi huu kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

(i) Aina za dosari zinazoweza kujitokeza katika mchakato mzima wa ujifunzaji lugha.

(ii) Jinsi ya kuainisha dosari hizo

(iii) Jinsi ya kurekebisha dosari zinazotolewa wa wajifunzaji wa lugha ya pili

**11.** Taja mambo muhimu matatu ya kuzingatia sana ili kufahamu vizuri habari ya kusikiliza.

**12.** Eleza tofauti ya ufahamu wa kusoma na ufahamu wa kusikiliza.

**13.** Zipo mbinu mahususi za kufundishia lugha na kwamba mbinu hizo zinaweza kusaidiwa na mbinu nyinginezo saidizi. Thibitisha usemi huu kwa kujenga hoja zenye mashiko huku ukirejelea mbinu saidizi katika kujifunza lugha kwa kuonyesha ubora na udhaifu wa kila mbinu.

# Marejeleo


Kipacha, A(2007) *Utangulizi wa Lugha na Isimu. Dar es Salaam:* Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Massamba, D.Kihore, Y. na Msanjila Y. (2004) *Isimu jamii. Sekondari na vyuo.* TUKI.

Masebo, J.A na Nyangwine, N,(2009) *Nadharia ya Lugha KISWAHILI 1* Nyamburi Nyangwine Publishers, Dar-Es Salaam, Tanzania.

Matinde S. R (2012), Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia. *Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu:* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wanjala F.S. na Kavoi J.M (2013), Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili: Kwa Wanafunzi, Walifunzi na Walimu. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Besha, R (1994), *Utangulizi wa Lugha na Isimu* . Dar es Salaam University Press.

Habwe, J. and Karanja, P (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi, Phonix Publishers

Massamba, D.Kihore, Y. na Msanjila Y. (2004) *fonolojia ya Kiswahili Sanifu (Fokisa) Sekondari na vyuo.* TUKI.

Nchimbi, A.S (2007) *OFC Kiswahili* Open University of Tanzania, Dar es Salaam

B. F. Skinner, (1957) *Sciense and Human Behavior*.The Macmillan Company: United States of America.

Kamusi Ya Kiswahili Sanifu, (1999**)** Institute of Kiswahili Research, Tanzania. Oxford University Press**.**

Masamba, (2009) *Kamusi ya Isimu na Lugha, Falsafa ya Lugha*.Tuki dar es salaam

Mgullu, R.S (1999) *Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*, Nairobi Kenya, Longhorn Publishers

N. Chomsky, (1957) Syntactic Structures. Schooneveld Indiana university Series minor Howard

P. Wang, (1995) *On the working definition of ittelligence*. Technical report 94.Center for research on concepts and cognition, Indiana University

Trudgill, P. (1974). *The Social Differentiation of English in Norwich*. Cambridge: CUP.

Wilder Penfield and Herbert Jasper: *Epilepsy and the Functional Anatomy of the Human Brain*: Boston, Little Brown and Co; 1957.

W i l d e r Penfield and Theodore Rasmussen, (1957) *The Cerebral Cortex of Man. A Clinical Study of Localization of Function*: N e w York, Macmillan;

Wilder Penfield and Lamar Roberts, (1959) *Speech and Brain Mechanisms*: Princeton, Princeton University Press.

W.V. Bingham, (1937) *Aptitudes and Aptitude Testing*. Herper &Brothers Newyork.